**ASKOFU** ataka ulinzi watoto wa kiume dhidi ya baa ushoga

UKURASA 3



**KIKAO** upatanishi usiku kilivyotatua migogoro ya ardhi

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Julai 8, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581365

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo

# Polisi adaiwa kuua kijana kwa kumpiga risasi 3 barabarani

**NDUGU** wagoma kuzika mwili, wajiapiza kuupeleka nyumbani kwa askari huyo...*Endelea ukurasa 15*

Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na mwenyeji wake, Rais wa Malawi, Dk. Lazarus Chakwera, wakishuhudia wakati Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kulia), akibadilishana hati na Waziri wa Habari na TEHAMA wa Malawi, Moses Kalongashwa, baada ya kutia saini mkataba wa makubaliano ya ushirikiano kati ya nchi hizo mbili kwenye TEHAMA, Lilongwe jana. **PICHA: IKULU**



# Samia aomba wakuu wa nchi Kiswahili kiwe somo

UKURASA 2

## DC, polisi wavunja ndoa mwanafunzi aliyeozeshwa kwa mahari ya 30,000/-

UKURASA 2

**MICHEZO** **NKANE KUTIBIWA NA SERIKALI** UK. 24 **KATUNI** UK. 6




Waziri wa Nashati, January Makamba (katikati), akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano kati ya serikali ya Tanzania na Zambia kuhusu utanuzi wa bomba la mafuta, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Ulinzi wa Zambia, Ambrose Lufuma na Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia aomba wakuu wa nchi Kiswahili kiwe somo

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan katika kuadhimisha Siku ya Kiswahili Duniani, ametoa wito kwa wakuu wa nchi duniani na serikali zao kuhamasisha kufundisha lugha ya Kiswahili katika nchi zao kwa kuwa matumizi yake ni mapana zaidi na yenye tija.

Akitoa salamu zake jana katika kuadhimisha Siku ya Kiswahili Duniani, Rais Samia alisema maadhimisho hayo hayakuja kwa bahati mbaya, yametokana na mchango uliofanywa na wanazuoni, wanaharakati na watafiti mbalimbali.

"Ndugu wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili popote mlipo duniani, ninawapongeza wote mnaoadhimisha Siku ya Kiswahili Duniani. Ahadi ya Watanzania kwenu ni kuyafanyia kazi maazimio yatakayoibuliwa katika majukwaa mbalimbali yanayohusiana na matumizi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili," alisema.

Mkuu wa Nchi alisema wanazuoni, wanaharakati na watafiti mbalimbali kwa moyo wao wa dhati waliandaa andiko kwa kujenga hoja na kuonesha ushahidi kwamba Kiswahili si lugha tu ya Tanzania, Afrika Mashariki na nchi za maziwa makuu, bali pia ni lugha ya Afrika na iliyoenea duniani kote.

Alisema hoja zao ndizo zilizowezesha Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) wakati wa mkutano wa 41 wa nchi wanachama uliofanyika mwezi Novemba mwaka juzi Ufaransa, kufanya uamuzi wa Siku ya Kiswahili Duniani.

"Niwapongeze wote walioshiriki katika kufanikisha kufanya uamuzi wa kuwa na Siku ya Kiswahili Duniani. Ndugu zangu Watanzania na wazungumzaji wa Kiswahili, ni ukweli baadhi ya mifarakano na migongano inayojitokeza duniani inachangiwa kwa kutokuwapo kwa lugha inayounganisha jamii na kuleta maelewano,"alisema.

Rais Samia alisema kwa upande wa Tanzania, wanafarijika kuwa na umoja na mshikamano unaochangiwa na kuwa na lugha ya kitaifa inayounganisha Watanzania na kuleta amani na utulivu na kuchangia kujenga Taifa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

"Jukumu ya kukiendeleza na kukipigania Kiswahili ili kipae zaidi kimataifa lipo mikononi mwetu. Kukua kwa matumizi ya Kiswahili duniani kumeibua mataifa ambayo yameamua kutumia lugha hii. Hiyo ni fursa ya Watanzania kufundisha Kiswahili katika mataifa hayo.

Aliwahakikishia kwamba serikali imeweka mikakati ya kuhamasisha Watanzania wenye weledi katika lugha hiyo kuchangamkia fursa zitokanazo na kukua kwake kama vile ukalimani, tafsiri, uhariri, uandishi wa habari, uandishi wa vitabu, utangazaji na ufundishaji Kiswahili kwa wageni, hata utungaji na uimbaji wa nyimbo na muziki.

Alisema Kiswahili kwa sasa kinatumika katika mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU), hivyo Tanzania kama kitovu hawana budi kukipa nguvu na kuongeza matumizi yake katika nyanja za kiuchumi, kidiplomasia, sayansi na teknolojia.

"Ninapendekeza kaulimbiu ya Siku ya Kiswahili Duniani kwa mwaka 2023 iwe 'Kiswahili ni Zaidi ya Lugha'. Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imeandaa mkakati wa taifa uliozinduliwa Julai 7, mwaka 2022 wenye lengo la kuifanya lugha hiyo kuwa bidhaa itakayouzika duniani kote.

**MKUTANO CCM**

Katika hatua nyingine, mwandishi wetu Beatrice Shayo, anaripoti kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia leo anatarajiwa kuongoza kikao cha Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kitakachofanyika jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na kutiwa saini na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Sophia Mjema, ni sehemu ya vikao vyao wa kawaida vya uongozi wa chama ngazi ya Taifa.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa vikao vya Kamati Kuu (CC) ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) Taifa vitafanyika kuanzia kesho jijini Dodoma.

"Vikao hivyo vya kawaida vya uongozi wa chama ngazi ya Taifa vitafanyika kwa mujibu wa Katiba ya CCM ya Mwaka 1977, Toleo la 2023, vikitanguliwa na kikao cha Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa itakayoketi Julai 8, mwaka huu (leo)," ilielezwa katika taarifa hiyo.

## DC, polisi wavunja ndoa ya mwanafunzi na muuza urembo

**Na Beatrice Shayo**

MWANAFUNZI wa kidato cha tano katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi (jina tunalo) ameozeshwa na wazazi katika Kijiji cha Chingulungulu, Kata ya Muhuwesi, wilayani Tunduru mkoani Ruvuma.

Inadaiwa kuwa wazazi wake wamemwozesha kwa 'muuza urembo' ndoa ya kimila kwa mahari ya Sh. 30,000.

Ndoa hiyo ambayo ilifungwa mwezi Aprili mwaka huu huku binti huyo akiwa amechaguliwa kuingia kidato cha tano, ilivunjwa usiku wa kuamkia jana na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro.

Kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi mkoani humo linawashikiliwa watu watano akiwamo mwoaji Mohamed Salum (32), maarufu Muddy muuza urembo, mkazi wa Kijiji cha Muungano mjini Tundumu.

Wengine ni baba wa mwanafunzi huyo, dada wa binti huyo ambaye ndiye anatajwa kuwaunganisha uchumba huo na binti mwingine aliyekuwa miongoni mwa washenga.

Akizungumzia tukio hilo, Mtatiro alisema amevunja ndoa hiyo iliyofungwa kinyemela baina ya Muddy na mwanafunzi huyo.

Mtatiro alisema aliongoza vyombo vya usalama kuwakamata wazazi waliomwozesha binti huyo na washenga waliohusika katika tukio hilo.

Alisema kijana huyo alikamatwa usiku wa kuamkia jana akiwa anaishi na mwanafunzi huyo katika Kijiji cha Muungano, Tunduru.

"Mzazi wa binti amekiri kumwoza binti yao kwa mahari ya Sh. 30,000 kwa madai kuwa binti hakuwa tayari kuendelea na elimu yake ya kidato cha tano," alisema.

Mtatiro alisema alipomhoji mwanafunzi huyo alisema yuko tayari kuendelea na masomo yake ikiwa atapewa nafasi hiyo.

Mtatiro alisisitiza binti huyo atasimamiwa aendelee na masomo yake na kuendeleza ndoto zake kielimu.

"Nimemkabidhi binti huyu kwa taasisi inayolea na kufadhili mamia ya wanafunzi wilayani Tunduru inayojulikana kwa jina la Kalamu Education Foundation (KEF), ili kufanikisha msichana huyo kuendelea na masomo," alisema.

Kiongozi huyo aliwataka wazazi kuacha mambo ya kizamani ya kuozesha mabinti ambao wana nafasi ya kuwa na mchango mkubwa zaidi kwa Taifa.

Alisema watuhumiwa watano wanashikiliwa na polisi wilayani huko kwa mahojiano kutokana na tuhuma za kula njama na kumwoza binti huyo.

Makamu Mwenyekiti wa KEF ambaye pia ni Diwani wa Masonya wilayani Tunduru, Said Bwanali, alikiri kuwa na taarifa kuhusu tukio hilo na kuahidi kuwa taasisi yao itamsimamia binti huyo.

# Askofu ataka ulinzi watoto wa kiume dhidi ya ushoga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, amewataka wazazi na walezi nchini kujenga misingi imara ya imani na maadili kwa watoto wao na kuwalinda dhidi ya ushoga.

Kiongozi huyo wa kiroho alitoa rai hiyo juzi wakati wa sherehe za kumpa daraja la upadre James Mrema wa Parokia ya Mwadui wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.

Alisema wazazi wanapaswa kuwa karibu na watoto wao. Wafuatilie mienendo yao ili kuwaepusha na janga la ushoga, alilolitaja sasa linachochewa kwa nguvu kubwa na makundi mbalimbali yakiwamo baadhi ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.

"Vitendo vya ushoga vikifumbiwa macho vitavuruga familia na ustawi wa jamii, ikiwamo wito mtakatifu wa upadre ambao unatoka katika familia," alisema Askofu Sangu.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Chistina Mndeme, aliwataka kinamama kuhakikisha wanasimamia malezi bora ya watoto, huku akiitaka jamii kuyakataa na kuyakemea mambo yote yasiyofaa zikiwamo mila mbaya. Christina alisema serikali inaheshimu, kutambua na kuthamini kazi zinazofanywa na taasisi za kidini likiwamo Kanisa Katoliki kupitia huduma mbalimbali za kijamii katika sekta za afya, elimu, maji na kilimo.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na taasisi zote za dini kwa ajili ya ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.

Mkuu wa Mkoa huyo pia aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kuombea amani ya taifa pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan ili Mungu amlinde katika majukumu yake ya kuliongoza taifa.



Mmoja wa waongozaji wa Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam, Ezbon Kashaga (mbele), akifafanua jambo kwa wanafunzi na walimu wa shule ya awali na msingi ya Sister Paulin Bommer ya Kibaha mkoani Pwani, walipotembelea kijiji hicho jana, kujifunza mambo mbalimbali. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wawekezaji 40 wa India watua nchini kusaka fursa

**Na Joseph Mwendapole**

UJUMBE wa wawekezaji 40 kutoka India uko nchini kutafuta fursa mbalimbali za uwekezaji, ukikutana na wafanyabiashara wa ndani.

Wawekezaji hao wameonesha nia ya kuwekeza katika sekta za afya, elimu, madini, mafuta, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na nishati jadidifu.

Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) jana kiliandaa mkutano baina ya wawekezaji hao na wenzao wa nchini uliofanyika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Kiongozi wa ujumbe huo, Rekha Sharma, alisema wako nchini kwa ajili ya kuangalia maeneo ambayo wanaweza kuwekeza.

Alisema kwa mujibu wa maelezo waliyopewa na Mkurugenzi Mkuu wa TIC, mazingira ya uwekezaji kwa sasa nchini yanavutia na watawekeza katika maeneo mbalimbali ikiwamo madini na kuahidi kuwashawishi wenzao kuja.

"Tuko nchini Tanzania tangu Julai 5, tumetoka maeneo mbalimbali ya India, wengine wametokea Mumbai, Gujarat, tumekuja kuangalia mazingira ya uwekezaji na nini tunachoweza kuwekeza hapa," alisema.

Aliongeza kuwa wawekezaji hao wa India wanatoka sekta za madini, mafuta, elimu na afya. Wamefurahishwa na maelezo ya Mkurugenzi Mkuu wa TIC kuhusu namna mazingira ya uwekezaji nchini yalivyo rafiki kwa wawekezaji wa kigeni.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Oman Said Shaaban, alisema Tanzania na India ni marafiki wa muda mrefu na wamekuwa wanafanya biashara za fedha nyingi.

Alisema ili kuhakikisha pande hizo mbili zinanufaika na ushirikiano huo, mwaka 2000 waliamua kuunda tume ya pamoja ambayo kazi yake ni kuwezesha utekelezaji wa makubaliano ya biashara baina ya India na Tanzania.

"Kama mnavyofahamu Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi na imeweka mazingira rafiki kwa wawekezaji ambayo yawavutia wawekezaji wa kigeni na takwimu zinaonyesha kuwa kiwango cha biashara baina yetu na India kimeongezeka kutoka dola za Marekaani milioni 2,836.40 mwaka 2013 hadi dola milioni 3,138.9 mwaka 2022," alisema.

# Maofisa rasilimali watu wapewa angalizo mchango wa wafanyakazi

**Na Romana Mallya**

MAOFISA rasilimali watu na viongozi wa biashara wamekumbushwa ni chachu ya kusaidia taasisi na mashirika kufikia mafanikio kwa kuwaona wafanyakazi kama wadau au wabia wa maeneo wanayoyaongoza.

Ni rai iliyotolewa jana mkoani Dar es Salaam wakati wa mkutano wa maofisa rasilimali watu na viongozi wa biashara uliowakutanisha pia viongozi mbalimbali na watoa mada kutoka Bangladesh na Dubai.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Epvate and Fortune International Consulting (EFIC), Peter Mapigano, alisema kazi yao kubwa ni kusaidia taasisi mbalimbali kuwa na ufanisi mahala pa kazi na kuandaa sera na mipango mikakati na miongozo na masuala ya kiteknolojia katika uendeshaji wa taasisi.

"Tupo hapa kuwakumbusha viongozi kwamba wana jukumu kubwa la kusaidia taasisi zao kufikia ndoto au matamanio ya taaasisi walizozianzisha.

"Watu karibu 200 wamekutanishwa na wazungumzaji wakubwa kutoka Bangladesh na Dubai pamoja na viongozi mbalimbali. "Tumewakutanisha na meneja rasiliamali watu na maofisa utumishi ambao hawa ndio chachu ya kusaidia taasisi kufikia mafanikio," alisema.

Mapigano alisema idara ya rasilimali watu ndio ya kwanza na ya pili kwa muhimu katika taasisi au kampuni yoyote, hivyo wameona wawapatie fikra mpya, kwamba wanapaswa kuiangalia rasilimali watu kwa namna tofauti kwenye maeneo yao.

"Watu watambue kwamba kuwa na mitambo, mashine au magari haitoshi kusaidia taasisi kufikia malengo. Watu wako ni wa muhimu kuleta mabadiliko. Na mabadiliko yanaanza na wewe kama kiongozi ili uweze kufanya taasisi yako ifikie maendeleo uliyokusudia," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuna haja kuangalia wafanyakazi kwa namna tofauti na kuwakumbusha kwamba wanapopata kiasi wakirejeshe kwa kundi hilo na wawafikirie kama ni wadau au wabia ndani ya taasisi zao.

Balozi mstaafu Peter Kallaghe ambaye alikuwa miongoni mwa washiriki wa warsha hiyo, alisema rasilimali watu ni muhimu katika mafanikio ya taasisi yoyote ya umma na sekta binafsi.

"Swali la kujiuliza - tumewaandaje vijana wetu na kazi na madaraka au majukumu ambayo yapo? Tupo kwenye ulimwengu wa ushindani kama nchi, ni kwa namna gani tunawajenga vijana wafanye kazi kwenye sekta ya umma au sekta binafsi?" alihoji. Alisisitiza fani hiyo ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa, hivyo ni lazima vijana waandaliwe vizuri.

Getrude Sima kutoka Shirika la Kazi Duniani (ILO), anayeratibu shughuli za Afya na Usalama Mahali pa kazi na kushughulikia masuala ya kijinsia na UKIMWI, alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa wao wana jukumu kubwa la kutengeneza mikataba mbalimbali kwa kushirikiana na wadau.

"Mkutano huu unalenga watu wawe sehemu ya kuleta maendeleo katika maeneo yao ya kazi. ILO tunathamini sana wafanyakazi, ndio maana tunashirikiana na nchi wanachama ikiwamo Tanzania kuhakikisha mikataba hii inatekelezwa na kuhushwa pahala pa kazi," alisema.

Alitoa wito kwa wadau kupitia vyama vyao, kikiwamo Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), kuendelea kukaa na kutoa vipaumbele kwa masuala ya majadiliano ya pamoja ili kuboresha ulimwengu wa kazi ambao kwa sasa unakumbwa na changamoto mbalimbali.

Alizitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na watu kuhama na kwenda kutafuta kazi sehemu zingine na kuathiri ulimwengu wa kazi.

Changamoto zingine alizitaja ni ugonjwa wa UVIKO-19 ambao umeleta changamoto katika uzalishaji na afya za wafanyakazi, pia mabadiliko ya tabia nchi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha CHAMWINO**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 16/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU DADI RAMADHANI KAMBI wa KASANGA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWANAID SHOMARY KAMBI**

**TANGAZO**

***(kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **19** Mwezi **07** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 27 mwezi 06 mwaka 2023

HAKIMU
MOROGORO



Mgombea udiwani wa Kata ya Potwe, wilayani Muheza mkoani Tanga kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Othuman Bahari Papa, akizungumza wakati wa ufunguzi wa kampeni ya CCM ya uchaguzi kwenye viwanja vya Mwembeni, Kijiji cha Ndondondo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kikao cha upatanishi usiku chatatua migogoro ya ardhi

## ●Wataalamu walioichochea waitwa kujieleza

**Na Moses Ng'wat,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael, ametatua migogoro ya ardhi iliyodumu kwa zaidi ya miaka 20 kati ya Halmashauri za Wilaya ya Mbozi, Halmashauri ya Mji Tunduma na wananchi kwa kufanya kikao cha utatuzi hadi majira ya usiku.

Dk. Michael aliitisha kikao hicho jana baada ya wananchi kuwasilisha malalamiko hayo ofisini kwake, wakilalamikia halmashauri kuchukua maeneo yao ya asili na kuwauzia watu wengine pasipo kulipa fidia.

Katika kikao hicho ambacho kilihudhuriwa pia na Kamishna wa Ardhi Tanzania, Mathew Nhonge, kilitatua migogoro mikubwa mitatu iliyowasilishwa katika ofisi hiyo ya Mkuu wa Mkoa, ukiwamo wa kiwanda cha saruji cha Mbeya na wananchi wa Kijiji cha Nanyala wilayani Mbozi uliodumu kwa zaidi ya miaka 20 licha ya viongozi mbalimbali wakiwamo wakuu wa mikoa waliopita kushindwa kuupatia suluhu.

"Tumekuwa na kikao kirefu, lakini kikao kizuri na leo tuliitana hapa ili tuweze kujadili na kutatua migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikisumbua kwa muda mrefu kwani nilipokuja hapa nilikuta kuna migogoro ya muda mrefu ambayo mingine ilianza tangu 1997, sasa ninashukuru Mungu tumehitimisha," alisema.

Dk. Michael alisema mgogoro wa kwanza ulikuwa kati ya Kiwanda cha Saruji cha Mbeya na wananchi wa Kijiji cha Nanyala ambapo katika majadiliano ya pamoja kati ya uongozi wa kiwanda na viongozi wa kijiji yamehitimishwa kwa makubaliano ya pande mbili kuridhiana na sasa mgogoro umemalizika.

"Kiwanda kilikuwa na tatizo kwani kilikuwa hakijapata hati na leo tumekaa na Kamishna wa Ardhi Tanzania (Nhonge) na baada ya kikao hiki, kiwanda (Mbeya Cement) watapewa ankara za malipo ya ardhi.

"Baada ya kulipia ankara za malipo ya ardhi, ninafikiri ndani ya wiki mbili kwa sababu hati tunazitayarisha hapahapa, watapata hati yao ili wananchi wa Nanyala waanze kupata maeneo kwa mikataba kadri watakavyokuwa wanakubaliana na kiwanda ili waanze kufanya shughuli za kiuchumi ikiwamo kulima au kuchimba chokaa," alifafanua zaidi Dk. Michael.

Mkuu wa Mkoa alisema migogoro mingine miwili ilihusu wananchi kutoka Halmashauri ya Mji Tunduma, ambao mama mjane Yusi Sikaponda, msimamizi wa mali za marehemu mumewe Ruben Sikaponda alilalamikia Halmashauri ya Mji wa Tunduma kupima eneo lake pasipo kulipwa chochote na kuwauzia watu wengine viwanja 70.

**"Kiwanda kilikuwa na tatizo kwani kilikuwa hakijapata hati na leo tumekaa na Kamishna wa Ardhi Tanzania (Nhonge) na baada ya kikao hiki, kiwanda (Mbeya Cement) watapewa ankara za malipo ya ardhi.**

Alisema baada ya majadiliano, mgogoro huo umefikia mwisho kwa Halmashauri ya Mji wa Tunduma ambayo wakati huo ikiwa sehemu ya Wilaya ya Mbozi kutakiwa kumlipa mjane huyo kiwango ambacho kimeridhiwa na pande zote mbili.

Mkuu wa Mkoa alisema mgogoro wa tatu ulihusiana na mgogoro wa kiwanja namba 465 (Kitalu A) ambapo mmiliki wa asili Khalfa Noti alikuwa katika mgogoro na Farid Masoud aliyemilikishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

Alisema kuwa baada ya majadiliano ya kina kuhusu mgogoro huo, pande mbili zilikubaliana. Halmashauri za Mji Tunduma na Mbozi zitamlipa mmiliki wa asili Noti Sh. milioni 100 kama fidia, huku Masoud naye akikubali 'kujazia' Sh. milioni 40.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa aliwaagiza wakurugenzi watendaji wa halmashauri hizo kuwaandikia barua za wito wa kurejea mara moja katika halmashauri hizo wataalamu wote wa ardhi wakiwamo waliostaafu wanaodaiwa kusababisha migogoro hiyo ili waje kujibu tuhuma na wakibainika kutenda makosa, wachukuliwe hatua.

## Waziri Mkuu: Wananchi watapata huduma afya katika maeneo yao

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inataka kuona wananchi wakipatiwa huduma za afya katika maeneo yao bila kulazimika kuzifuata mbali.

"Tumejenga vituo vya afya, hospitali za wilaya na sasa tunajenga hospitali katika kila halmashauri ili kusogeza huduma zaidi kwa wananchi. Nia ya serikali ni kuona wananchi wetu wanapata huduma muhimu hukohuko waliko," alisema jana mkoani Mtwara.

Ni kauli aliyoitoa baada ya kukagua ujenzi wa miundombinu na vifaa tiba katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini na Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Ligula) zilizoko mkoani Mtwara.

Akizungumza na watumishi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini, Waziri Mkuu, alisema malengo ya serikali ni kuifanya hospitali hiyo iwe mkombozi kwa wanakusini na nchi jirani za Msumbiji na Comoro.

"Rais Samia Suluhu Hassan anataka wananchi wasiende umbali mrefu kupata huduma, badala yake huduma zote ziishie hapo," Majaliwa alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali imeongeza fedha ya afya ili kufanya maboresho ya miundombinu na vifaa tiba vya kisasa katika maeneo yote ya utoaji wa huduma za afya.

"Hospitali hii imetengewa Sh. bilioni tatu za kuboresha miundombinu na vifaa tiba," alisema na kubainisha kuwa Hospitali hiyo ya Rufani ya Kanda ya Kusini, Mtwara itaendelea kupata huduma mpaka pale itakapokamilika ili malengo ya ujenzi wake yatimie.

Akitoa maelezo kwa Waziri Mkuu, Radiolojia Mkuu, Dk. Dennis Mosha, alisema hospitali hiyo imefanikiwa kusimika Mfumo wa Matibabu (eMedical HMIS) kwa ajili ya uhifadhi wa taarifa za matibabu. "Hospitali inatumia mfumo wa utunzaji wa picha za X- Ray, CT SCAN na MRI katika kuhakikisha utoaji bora wa huduma kwa njia ya kidijitali. Tunaweza kuwasiliana na MOI ili kupata ushauri zaidi wa kitaalamu endapo tunakwama," alisema.

Wakati huo, Waziri Mkuu ameweka jiwe la msingi la ujenzi katika Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Ligula) na kusema lengo la serikali ni kuona majengo hayo yanakamilika na hospitali inaanza kutoa huduma mara moja.

"Hatuhitaji kuona awamu za ujenzi zikichukua muda mrefu. Tunataka ujenzi uendelee ili ukamilike kwa haraka kwa sababu fedha zake zipo. Hakikisheni mkandarasi anamaliza jengo lote," aliagiza.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Lobikieli Kisambu, alisema ni la ghorofa moja. Litakapokamilika, litakuwa limegharimu Sh. bilioni 4.68. Hadi sasa zimekwishatumika Sh. bilioni 2.9.

"Jengo la chini (ground floor) limekamilika kwa asilimia 88," Mganga Mfawidhi alibainisha.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu jana alikagua mradi wa uboreshaji wa upatikanaji majisafi na salama katika chujio la maji lililoko Mangamba, linalosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara (MTUWASA).

Aliitaka Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini zifanye utafiti kwenye maeneo ambayo yanaweza kupatikana maji.

"Jukumu hili si lenu peke yenu, shirikianeni na viongozi wa halmashauri kuvibainisha na kuvilinda vyanzo hivyo ili dhamira ya Rais Samia ya kupeleka huduma za majisafi hadi kwenye vitongoji iweze kutimia," aliagiza.

Waziri Mkuu yuko ziarani mkoani Mtwara. Jioni alizungumza na wakazi wa Manispaa ya Mtwara.

# Mpango ahimiza wananchi waache kutumia kuni, mkaa

**Na Faustine Feliciane**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewahimiza watoa huduma za afya na wajawazito wilayani Buhigwe mkoani Kigoma, kutumia nishati safi ya kupikia ili kuboresha afya zao na kutokomeza matumizi ya kuni na mkaa.

Dk. Mpango amesema wakati umefika sasa kwa wananchi kuachana na matumizi ya vitu vinavyohatarisha afya zao wakati wa kupika.

Amesema matumizi ya nishati safi ya kupikia hayaepukiki na kuwataka watoa huduma za afya na wajawazito kuachana na matumizi ya kuni na mkaa ili kutunza mazingira, pia kuepuka matatizo ya kiafya.

"Wakati umefika sasa kwa wananchi kuondoka katika utaratibu wa matumizi ya kuni na badala yake sasa tutumie nishati ya gesi. Leo hii wenzetu wa ORYX wamefanya kazi nzuri sana ya kuwezesha wananchi hapa Buhigwe kupata gesi ya kupikia, ninawapongeza sana," alisema Dk. Mpango alipozungumza na wananchi huko Buhigwe juzi.

Makamu wa Rais aliishukuru kampuni ya ORYX kwa kutoa mitungi ya gesi 214 kwa wajawazito na mitungi 86 kwa watumishi wa afya ngazi ya jamii.

"Jamii sasa lazima ibadilike kwa kuhamia kwenye matumizi ya gesi safi katika kupikia. Hii itasaidia sana kutunza mazingira na kujali afya," alisema Dk. Mpango.

Meneja Mkuu wa ORYX Kanda ya Kaskazini, Alex John, akizungumza wakati wa kukabidhi mitungi ya gesi ya kupikia kwa watoa huduma za afya na wajawazito, alisema kampuni hiyo inaunga mkono jitihada za serikali za kuwapa fursa ya nishati safi kwa kiwango cha chini cha asilimia 80 wananchi ifikapo mwaka 2032.

"Huu ni mwendelezo wa jitihada za kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi wote.

Kampuni ya ORYX Tanzania muda huu imesimama na wananchi wa Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma kupitia Doris Molleli Foundation kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa watu wote," alisema John.

# 50 washikiliwa tuhuma uporaji wa simu, mikoba kwa pikipiki

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro linawashikilia watu 50 kwa tuhuma za uporaji wa simu na mikoba, wakiwamo wanaotumia pikipiki, maarufu vishandu.

Watuhumiwa hao walikamatwa kufuatia operesheni maalum ya kukamata wahalifu iliyofanywa na jeshi hilo kuanzia mwezi uliopita.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Hassan Omary, aliwataja baadhi ya watuhumiwa hao waliokamatwa ni pamoja na Hores Cliff (23), dereva wa bodaboda na mkazi wa Kihonda na wenzanke wawili ambao wanadaiwa kufanya unyang'anyi, wakitumia pikipiki yenye namba za usajili MC 227 DTW aina ya Haojue.

Pia, wamo Ricado Mchonde (23), dereva wa bodaboda na mkazi wa Kihonda Maduka Kumi na wenzake wawili wanaodaiwa kufanya unyang'anyi wa kutumia silaha wakiwa na pikipiki yenye namba za usajili MC 986 DFG. Wanadaiwa kupora mikoba yenye simu na vitu mbalimbali.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda huyo watuhumiwa wengine ni: Emmanuel Sanga, maarufu Imma The Boy (28), mkazi wa Kihonda Kwa Wagogo; Jackson Sihaba (27), bodaboda na mkazi wa Mwembesongo na wenzake wawili ambao wanadaiwa kufanya uhalifu huo kwa kukodishwa pikipiki na Ashraf Evance (21), bodaboda na mkazi wa Maduka Kumi.

Alibainisha kuwa katika operesheni hiyo, walikamata watu hao pamoja na pikipiki zaidi ya 60 zinazodaiwa kutumika kufanya uhalifu huo.

Alisema Jeshi la Polisi pia linamshikilia Shaban Abdul, maarufu Goha (42), fundi simu na mkazi wa Lukobe ambaye anadaiwa kununua simu hizo zilizoibiwa na vishandu.

Kamanda huyo alisema watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria. Aliutaja uhalifu huo umekuwa kero mjini Morogoro.

Kamanda huyo aliwataka wananchi kuendelea kuliamini jeshi hilo na kutoa ushirikiano katika kuendelea kupambana na wahalifu na kuwataka waathirika wa matukio hayo kufika katika kituo kikubwa cha polisi kwa ajili ya utambuzi wa simu zao.




Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Biashara ya Akiba (ACB), Silvest Arumas alipotembelea banda la benki hiyo, katika maonyesho ya 47 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MOI wapandikiza goti na nyonga bandia Zanzibar

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, Zanzibar wameendesha kambi maalum ya upasuaji wa kupandikiza goti na nyonga bandia.

Kupitia kambi hiyo, wagonjwa 16 wamefanyiwa upasuaji katika kipindi cha siku tano.

Kambi hiyo imefanyika ikiwa ni mwendelezo wa ushirikiano kati ya Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja na MOI wenye lengo la kusogeza huduma za kibingwa na kibobezi karibu na wananchi.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Marzui, akizungumza wakati wa kambi hiyo, alisema ni utekelezaji wa agizo la Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ally Mwinyi la kuhakikisha wananchi wanapata huduma za kibingwa na kibobezi bila kulazimika kuzifuata Dar es Salaam au nje ya nchi.

"Leo ni siku ya pekee kwani tumekutana hapa kueleza matunda ya ushirikiano kati ya Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja na MOI.

"Kama mnavyofahamu mwezi Novemba mwaka jana ushirikiano huu ulianza na leo tunashuhudia matunda yake ambapo madaktari bingwa na wauguzi kutoka MOI wamekuja Zanzibar kutoa huduma kwa wananchi wetu," alisema Mazrui.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, Dk. Muhiddin Mahmoud, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan na Rais Mwinyi pamoja na Waziri wa Afya Zanzibar, Mazrui, kwa usimamizi imara katika sekta ya afya.

Dk. Muhiddin alimshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Prof. Abel Makubi, kwa kuridhia kuanzisha ushirikiano na Hospitali ya Mnazi Mmoja - Zanzibar pamoja na kutuma jopo la madaktari wabobezi pamoja na wauguzi wabobezi kutoa huduma kwa wananchi wa Tanzania Zanzibar.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Violet Lupondo, alisema MOI imekua inatekeleza kwa vitendo maagizo ya serikali, likiwamo la kuhakikisha huduma za kibingwa zinasogezwa karibu na wananchi.

Alisema kuwa sasa huduma hizo zinatolewa katika maeneo mbalimbali nchini ili kuwapunguzia wananchi usumbufu wa kufuata huduma Dar es Salaam.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Alichofanya Rais Samia ni mfano wa kuigwa

**WIKI** hii klabu ya Yanga ilipata mwaliko wa heshima kutoka Serikali ya Malawi kwenda kucheza mchezo maalum wa kimataifa wa kuadhimisha Siku ya Uhuru wa nchi hiyo, walioupata mwaka 1964.

Mwaliko huo ulitoka kwa Rais wa nchi hiyo, Lazarus Chikwera ambaye alimwalika Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo ya kitaifa, ni heshima iliyoje.

Marais hao wote wawili walikuwapo kwenye Uwanja wa wa Bingu wa Mutharika kushuhudia mchezo huo wa kihistoria ambapo Yanga walicheza na wenyeji wao, Nyasa Big Bullets ya Lilongwe, Malawi.

Tukiachana na suala hilo la mwaliko, jambo kubwa ambalo linapaswa kuigwa ni maagizo ya Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa baada ya mchezaji wa Yanga, Denis Nkane kuumia wakati wa mchezo huo na kukimbizwa hospitali jijini humo.

Nkane aliumia baada ya kugongana na mchezaji wa Nyasa Big Bullets katika harakati za kuwania mpira na kusababisha kuzimia kwa dakika kadhaa, watu wa huduma ya afya walimpatia huduma kabla ya kumpeleka hospitali.

Baada ya kuona tuki hilo na kutambua ubalozi mwema wa Yanga kwenye shughuli hiyo, Rais Samia alitoa maagizo ya mchezaji huyo pindi atakaporejea nchini kupatiwa huduma ya afya kubaini ukubwa wa tatizo lake na kutibiwa kwa gharama ya serikali.

Kwa kitendo cha kutoa maagizo haya rais wetu ameonyesha uungwana mkubwa kwa kujali afya ya mchezaji ambaye alibeba taswira ya nchi kwenye shughuli ya majirani zetu Malawi.

Ni kweli Yanga ilienda Malawi kama klabu ya soka ya Tanzania na si kama timu ya Taifa, lakini kutambulika tu kuwa inatoka Tanzania kwenye shughuli ya Wamalawi tena mbele ya marais wa nchi zote maana yake Yanga ilikuwa balozi wa vilabu vingine vya Tanzania kwenye shughuli hiyo.

Maamuzi ya Rais ya kuagiza Serikali imtibu na kufuatilia afya ya Nkane ni maamuzi ya busara, maamuzi ya utu na ya kutambua heshima ambayo nchi imeipata baada ya Yanga kualikwa kwenda kucheza mchezo huo maalum ukiwa ndio mchezo wa kipekee wa kuadhimisha Uhuru wa nchi hiyo.

Kilichofanywa na Rais Samia kinapaswa kuigwa na taasisi yetu ya soka ambayo ina dhamana kubwa ya kusimamia na kuendeleza soka hapa nchini, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Tunazungumza hivi kwa sababu huko nyuma tumeshawahi kusikia malalamiko ya baadhi ya klabu zikiilalamika TFF kutojishughulisha na wachezaji wa klabu hizo pale wachezaji wao wanapuumia wakiwa kwenye majukumu ya timu za Taifa.

Ni wazi timu zetu za Taifa zinatakiwa kuwa chini ya Serikali, lakini linapokuja suala la afya ya mchezaji anapoumia chini ya mwamvuli wa TFF, basi ni vyema kuonyesha uungwana kwa kushiriki kwenye matibabu ya mchezaji huyo na si kuiachia mzigo klabu ya mchezaji husika.


Tulishawahi kusikia malalamiko ya beki wa pembeni wa Simba, Shomari Kapombe ambaye aliumia akiwa kwenye majukumu ya timu ya taifa na kulalamika uongozi wa TFF kumtelekeza na jukumu la kumtibu likabaki kwa klabu yake ya Simba.

Hali hiiilisababisha Kapombe kutangaza kustaafu kuichezea Taifa Stars kabla ya kubatilisha maamuzi hayo, inasemekana sababu kubwa ya kutangaza kustaafu ni namna TFF 'ilivyompotezea' kwenye matibabu yake.

Hili lililofanywa na Rais wetu Mama Samia ni la kuigwa, ameonyesha uungwana wa hali ya juu na mapenzi ya kweli kama Mama, lakini ameonyesha kwa vitendo namna gani anathamini na kupenda michezo.

Ni wazi michezo katika nchi hii sasa ipo kwenye mikono salama chini ya mlezi mama yetu, Rais Samia Suluhu Hassan.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera Bodi ya Ligi kukomalia wachezaji kupima afya lakini...

Na Adam Fungamwango

**KABLA** ya msimu wa mashindano kuanza, tunashuhudia klabu zikianza kupima afya za wachezaji.

Wachezaji wa klabu ya Simba walionekana kupima kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es Salaam huku wale wa Azam wakionekana kupima wachezaji wao Aga Khan.

Yote hiyo ni kuhakikisha kuwa wachezaji wanakuwa fiti na afya njema kwa ajili ya kuzitumikia klabu zao kwenye mashindano mbalimbali ya ndani na yale ya nje ya nchi nikimaanisha mashindano ya kimataifa, hii ni kujihakikishia mchezaji anakuwa fiti msimu mzima.

Hapa simaanishi kuwa hatoumia, hapana, ila ni kumwangalia mgonjwa kama ana matatizo au magonjwa mengine ya ndani ya mwili yasiyoonekana.

Tumeshuhudia matukio mengi ya wachezaji kuanguka uwanjani katika mechi au mazoezi na baada ya vipimo tunaambiwa mchezaji husika alikuwa na matatizo ya moyo au mengineyo yasiyojulikana kwa kumwangalia.

Daktari wa klabu ya Simba, Edwin Kagabo, aliweka wazi mchezaji anapaswa kutazamwa vipimo vyote muhimu kabla ya kuanza msimu mpya wa mshindano.

"Tunawapima wachezaji vitu muhimu vinavyohitajika kwa mchezaji kama uzito wa mwili, wingi wa damu, ufanyaji kazi wa figo na ini, ufanyaji kazi wa umeme kwenye moyo ili tufahamu utimamu wao kabla ya kuanza msimu," amesema Dk. Kagabo.

Wakati hayo yakiendelea, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) nayo ikazitaka klabu zote za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, na Daraja la Pili 'first league' kuwafanyia vipimo vya afya wachezaji wote watakaowatumia kwa msimu wa mashindano 2023/24 ili kutekeleza matakwa ya kikanuni na masharti ya leseni za klabu. Kwa mujibu Idara ya Habari na Mawasiliano ya bodi hiyo, ikasisitiza kuwa wachezaji wote watakaotumika kwa michezo ya ligi msimu ujao wanapaswa kuwa wamepimwa na kuthibitishwa na daktari kuwa hawana matatizo yoyote yanayoweza kuhatarisha usalama wao na wachezaji wengine.

"Wachezaji ambao hawatofanyiwa vipimo vya afya na kupata cheti cha utimamu wa afya, watakosa sifa za kusajiliwa na kupatiwa leseni maalum za usajili wa wachezaji zinazotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), hivyo hawatoruhusiwa kucheza mashindano yoyote yaliyo chini ya shirikisho hilo," ilisema taarifa hiyo.

Ikasema zoezi hilo ni muhimu na la lazima kwa mujibu wa kanuni ya 69:2 (2.4) ya Ligi Kuu, na ya 70:2.(2.4) kwa kanuni ya Ligi ya Championship na 'first league' kuhusu maombi ya usajili, hivyo klabu zote zinapaswa kuhakikisha zoezi hilo linafanyika kikamilifu chini ya daktari mwenye sifa na vigezo zinavyohitajika.

Mpaka hapa utaona kuwapima wachezaji si tu muhimu, lakini ipo kwenye kanuni za mashindano yanayosimamiwa na TFF.

Hii inaepuka kuwa na wachezaji ambao wana magonjwa kama vile ya moyo, ambapo husababisha kuweza kuanguka na kupata madhara makubwa ikiwamo hata kupoteza maisha.

Wachezaji ambao pia wana matatizo kiafya kuweza hata kusababisha hatari kwa wachezaji wenzao uwanjani, hivyo ni muhimu sana kuwapima wachezaji.

Hata hivyo nina shaka kama wachezaji wote wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanapimwa, kwanza mpaka sasa tumeona ni Simba na Azam tu ndiyo walioonyesha.

Inawezekana ikawa wachezaji wengine wanapimwa lakini hawaonyeshi, lakini kwa kuwaangalia tu baadhi ya wachezaji wengi wa Ligi Kuu nchini hawako fiti.

Naweza kusema ni kwa sababu tu ligi yetu haina kasi, vinginevyo ingekuwa balaa. Wachezaji wengi hawana pumzi na wanachoka mapema na wanapenda kucheza mechi taratibu mno, hii inaonyesha kuwa bado wana matatizo.

Wanatakiwa waangaliwe wanakula nini, aina ya mazoezi wanayofanya na mengine yanayofanana na hayo.

Soka la nguvu zisizokuwa na mpango, ubabe na kusukumana, linaonyesha kuwa bado wachezaji wetu wana matatizo.

Mchezaji ambaye hana utimamu wa mwili, na afya yake haijaimalika kwenye mikiki ya soka, ndiyo kwa kiasi kikubwa wanafanya kazi ya kumiza wenzao.

HABARI KITAIFA

# DC acharuka bonde kuvamiwa

**Na Halfani Chusi**

MKUU wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo, amepiga marufuku ujenzi katika Bonde la Kibada Block 1-4.

Amesema, eneo hilo ni mali ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Liko Kata ya Kibada, Mtaa wa Kichangani.

Kiongozi huyo alitangaza marufuku hiyo juzi alipotembelea eneo hilo na kusikiliza kero za wananchi. Aliagiza wananchi waliojenga katika eneo hilo kufika ofisini kwake ndani ya siku 14 ili kupata maelekezo.

Alisema kumekuwapo kwa taarifa ya baadhi ya watu kuvamia maeneo na kuyaendeleza bila rukhsa, jambo ambalo limekuwa linazua taharuki kila kukicha.

"Marufuku mtu kuvamia eneo, asijenge mtu yeyote hadi majibu kutoka wizarani yapatikane na manispaa waangalie nini cha kufanya. Kamati ya Fedha ya Manispaa inakuja kukagua maeneo kubainisha ni yapi yamevamiwa na mabonde yalipopimwa.

"Nimesikia wauzaji mabonde na viwanja vya wazi ni baadhi ya wakazi na viongozi wa mitaa. Ninaomba nipewe majina niwashughulikie," aliagiza.

Awali akiwasilisha kero kwa niaba ya wakazi wa eneo hilo, Sostenes Sambua, alisema uvamizi wa viwanja Block 1-4 na eneo la NSSF umesababisha kuwapo wezi mchana na usiku.

Pia kumekuwa na migogoro na wamiliki ambayo hata watangulizi wake wawili waliopita, iliwawia ugumu kuitatua.

Kabla ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni hivi karibuni, Halima alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

"Upimaji wa mabonde baada ya mradi wa viwanja 20,000 kukabidhiwa manispaa, umekiuka taratibu. Wakazi hawakuhusishwa. Serikali ya mtaa haikuhusishwa na manispaa haikuhusishwa.

"Baadhi ya maofisa wa Wizara ya Ardhi wamebadilisha matumizi ya mabonde, wamepunguza ukubwa wa barabara, baadaye wakishajenga kutatokea mafuriko kama ya Tabata na Mto Msimbazi," alionya.

Alisema maeneo ya wazi katika mitaa yanabadilishiwa matumizi na kumilikishwa watu binafsi, hivyo kuwanyima watoto haki ya kucheza. Wazee nao hawana sehemu za michezo na mazoezi.

Ni hoja ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aliichambua kwa kina kupitia ripoti yake ya Ukaguzi Maalum wa Maeneo ya Wazi nchini ya Machi 2017, akitoa hoja kwamba maeneo mengi yamevamiwa na kuendelezwa.



Mbunge wa Jimbo la Nachingwea, mkoani Lindi, Dk. Amandus Chinguile (wa pili kulia), akizungumza baada ya wajumbe wa kamati ya siasa ya CCM ya wilaya ya Nachingwea, kukagua mradi wa ujenzi wa maabara ya shule ya sekondari Namatula, kata ya Namatula juzi, unaoghalimu kiasi cha Sh. milioni 30. Wa (tatu kulia) ni Mkuu wa wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dereva anayedaiwa kusababisha ajali iliyoua ndugu wanne akamatwa

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

JESHI la Polisi mkoani Mtwara limemkamata dereva wa lori, Shabani Hassani (37), mkazi wa Moshi mkoani Kilimanjaro, anayedaiwa kusababisha vifo vya watu wanne.

Ndugu hao walipoteza maisha walipokuwa wamepakiana kwenye pikipiki wakitokea mjini Masasi kuelekea Kijiji cha Lupaso wilayani Masasi.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Nicodemus Katembo, alilithibitisha kukamatwa kwa dereva huyo. Ni baada ya jeshi hilo kufanya msako.

Alisema kuwa, dereva huyo ambaye alikuwa anaendesha lori lenye namba za usajili T 522 BBQ aina Fuso anadaiwa kusababisha vifo vya watu wanne ambao ni ndugu wa familia moja baada ya kuigonga pikipiki yenye namba za usajili MC- 406 aina ya TVS na kusababisha vifo vyao.

Kamanda Katembo alikumbusha kuwa ajali hiyo ilitokea wilayani Masasi, Mtaa wa Napupa, Kata ya Napupa barabara iendayo wilayani Newala na kusababisha vifo hivyo.

Alisema kuwa baada ya ajali, dereva wa lori hilo alikimbia na ndipo Jeshi la Polisi lilipofanya msako na kumkata.

Alisema uchunguzi wa chanzo cha ajali hiyo uliofanywa na Jeshi la Polisi, umebaini ilitokana na uzembe wa dereva wa lori kuingia upande ambao sio wake na kushindwa kukwepa vyombo vya moto vingine.

"Tunamshikilia dereva wa lori Shabani Hassani (37), mkazi wa Moshi, kwa kusababisha vifo vya watu wanne ambao ni ndugu wa familia moja, wakazi wa Kijiji cha Lupaso.

"Tunatarajia kumfikisha mahakamani hivi karibuni kwa makosa ya uzembe wakati akiendesha lori hilo," alisema Kamanda Katembo.

Kamanda huyo aliwataja waliopoteza maisha katika ajali hiyo iliyotokea wiki iliyopita wilayani Masasi ni Danrford Milanzi (29), Rashford Milanzi (6), Omega Danford (23) na Norah Mrope (22).

Alisema wanafamilia hao waliofariki dunia kwa kugongwa na lori hilo, wote ni wakazi wa Kijiji cha Lupaso wilayani Masasi.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa watumiaji wa vyombo vya moto kuwa waangalifu wanapoendesha vyombo hivyo.

Kamanda Katembo pia alisema Jeshi la Polisi mkoani Mtwara litaendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa vyombo vya moto ili kila moja atii sheria na kanuni za usalama barabarani jambo ambalo litapunguza ajali ambazo ni za uzembe.

Alisema kwa sasa dereva huyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kusababisha vifo vya watu hao wanne. Taratibu za upelelezi zikikamilika, atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yatakayofunguliwa dhidi yake.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



# Kituo kipya mikutano kimataifa kujengwa

**Na Restuta James**

SERIKALI inakusudia kujenga kituo kikubwa cha mikutano cha kimataifa kitakachopewa jina la Mlima Kilimanjaro, ikiwa ni mkakati wa kuvutia utalii wa mikutano nchini.

Katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa maarufu Sabasaba, Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), Ephraim Mafuru, alisema jana kuwa uamuzi huo umefikiwa baada ya kufanya tathmini ya fursa za utalii wa mikutano nchini na barani Afrika.

Alisema AICC inaboresha kumbi zake za Arusha na Julius Nyerere, Dar es Salaam kwa kuweka mifumo inayoendana na soko la utalii huo.

"Lakini ambalo ni kubwa, tutawekeza katika kituo kikubwa kabisa cha mikutano kitakachoitwa Mount Kilimanjaro International Convention Centre. Kitajengwa Arusha. Tuna ardhi ya ekari 90, tutajenga ukumbi mkubwa wa kisasa ambao hautakuwa na nguzo katikati utakaoweza kuchukua watu 3,000 kwa wakati mmoja," alisema.

Mafuru alisema kituo hicho kitakuwa na eneo la maonesho lenye ukubwa wa mita za mraba 10,000, hoteli mbili zenye hadhi ya nyota tano, zitakazolaza wageni 1,000 kwa mara moja na nyumba za marais (presidential suits).

"Tunajiuliza hivi tukipokea marais 50 kwa mara moja, tutawalaza wapi? Kwa hiyo, kituo cha AICC kitawekeza katika nyumba bora za kisasa kwa ajili ya kuwakaribisha marais hapa Tanzania," alisema.

Alibainisha kuwa kituo hicho kitawekeza pia katika eneo la ununuzi (shopping mall), ambalo litajengwa Kijenge jijini Arusha kwa ajili ya wafanyabiashara wanaotaka kuuza bidhaa zao na eneo la michezo ili watalii wa mikutano wapate huduma zote muhimu sehemu moja.

Mafuru alisema filamu ya Tanzania The Royal Tour imeipandisha Tanzania katika utalii wa mikutano Afrika kutoka nafasi ya 11 hadi nafasi ya tano mwaka jana.

Alibainisha kuwa mwaka jana, AICC ilitoa huduma kwa mikutano 18 ya kimataifa na mwaka huu tayari wameshahudumia mikutano 150 ya kitaifa na kimataifa.

Alisema wiki mbili zilizopita, kituo hicho kilitoa huduma kwa mkutano mkubwa wa kidunia wa wataalamu wa afya ambao ulihudhuriwa na watu 1,200. Kati yao, 1,000 walitoka nchi 107 duniani.

Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alisema Tanzania ina nafasi ya kuendelea kufanya vizuri katika utalii wa mikutano, akieleza kuwa ameshafanikisha kuleta nchi mikutano miwili ya kimataifa na Desemba mwaka huu, mkutano wa kimataifa wa Global Partnership for Education utafanyika nchini.




Ofisa Uhusiano wa wanahisa wa Kampuni ya Uwekezaji ya NICOL, Irene Nkya (kushoto), akiwahudumia baadhi ya wateja waliofika kwenye banda lao katika maonyesho ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam Uwanja wa Mwalimu Nyerere, barabara ya Kilwa jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Makubaliano mradi wa gesi asilia yafikia pazuri

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Timu ya Majadiliano kwa upande wa Serikali ya Tanzania katika utekelezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG), Charles Sangweni, amesema wamefikia hatua nzuri katika maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo.

Sangweni alitoa kauli hiyo jana katika banda la PURA katika Maonesho ya Sabasaba mkoani Dar es Salaam. Wameingia mikataba mitano ya utekelezaji wa mradi huo.

Alisema mkataba wa kwanza waliokubaliana ni wa nchi hodhi ambao umeanisha misingi ya uwekezaji, ugawanaji na utekelezaji wa mkataba wenyewe.

Alitaja mikataba mingine ni ya ugawanaji mapato utakaoendana na mradi (PSA), mkataba wa ukodishaji ardhi, mkataba wa namna ya kutumia Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwenye masuala ya bandari na mkataba wa ulinzi wa miundombinu ya mradi.

Alisema, majadiliano kuhusu utekelezaji wa mradi huo yalianza mwaka 2021 na yalimalizika Mei 19 mwaka huu. Kila mshirika aliondoka na kile kilichojadiliwa kupeleka katika mamlaka za uamuzi za upande wake kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi.

"Mimi ndiye nilikuwa mwenyekiti wa timu ya majadiliano upande wa Serikali ya Tanzania. Mazungumzo haya yalihusisha makubaliano ya mikataba mitano.;

"Mkataba wa pili tuliona kwamba kwa kuwa tunaenda kwenye uhalisia wa utekelezaji wa mradi, tulisema ni vyema tuwe na mkataba wa ugawanaji mapato utakaoendana na mradi (PSA), kwa kuboresha.

"Lakini tulijadiliana juu ya mkataba wa ukodishaji ardhi ambayo itajengwa mitambo itakayokuwa inamilikiwa na TPDC (Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania).

"Tukumbuke kwamba gesi hii itasafirishwa kwenda nchi za mbali kwa kutumia meli maalum zenye uwezo wa kubeba LNG, kwa hiyo pia tulifanya makubaliano ya ulinzi wa miundombinu ambayo itajengwa," alisema.

Alikumbusha kuwa mradi huo wa LNG unatarajiwa kugharimu Sh. trilioni 97. Watanzania zaidi ya elfu 10 watapata ajira.

# Vitongoji 36,000 kufikiwa na umeme ifikapo 2030

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI wa Huduma za Ufundi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Jones Olutu, amesema ifikapo mwaka 2030, vitongoji 36,000 ambavyo havina umeme nchini, vitakuwa vimepata nishati hiyo.

Alitoa ahadi hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya Sabasaba yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam.

Olutu alisema ifikapo mwaka 2030 ambao ni ukomo wa upimaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, vitongoji 64,760 vitakuwa vimepata umeme. Mpaka sasa vitongoji 28,000 vimeshapatiwa huduma hiyo.

"Vitongoji 36,000 vilivyobaki navyo vipo katika mpango, yaani kwenye hatua za utekelezaji na tuna matumaini kuwa ifikapo 2030, tutakuwa tumevimaliza vyote. Tukimaliza hili, maisha ya vijijini yatakuwa sawa na mijini kwani fursa na biashara ambazo zitatumia umeme zitakuwa nyingi," alisema.

Olutu alisisitiza kukamilika kwa mipango hiyo kutachagiza kila mradi uliopo kijijini uwe wa maji, vituo vya afya na mingine ya kimaendeleo, kufikiwa na umeme.

Alibainisha kuwa vijiji 10,125 kati ya 12,318 vya Tanzania Bara, tayari vimeshapatiwa huduma ya umeme na vilivyobaki ifikapo Desemba mwaka huu vitafikiwa na nishati hiyo.

Alisema kuwa katika maonesho hayo wamejipanga kuonesha miradi mbalimbali ambayo wameitekekeza na mafanikio yaliyopatikana. Watawaeleza wananchi namna bora ya kutumia nishati ya umeme kujipatia kipato.

Olutu alisema miradi wanayoitekeleza inalenga kuinua maisha ya watanzania na REA itawawezesha watanzania kupata mikopo yenye riba nafuu ya asilimia tano ili kujikwamua kiuchumi.

"Tunatoa mkopo kiasi cha Sh. milioni 70 ambacho kinaweza kumsaidia mtu kuanzisha kituo kidogo cha kuuza mafuta na kupata mtaji wa kuweka mafuta na kuendesha maisha na wengi wao wamefika hapa kutaka kujua namna ya kuupata mkopo huo.

"Watanzania wote wenye uhitaji wafike bandani kwetu. Watapatiwa vigezo na masharti ya kupata mkopo huo na wataelezwa namna ya kujaza maombi yao ili kupatiwa mkopo huo," alisema.

# NICOL yawaita wanahisa Sabasaba kupata gawio

**Na Joseph Mwendapole.**

KAMPUNI ya Uwekezaji ya NICOL imesema imeendelea kufanya vizuri sokoni kwa kupata ongezeko la faida ya Sh. bilioni 6.2 mwaka huu kulinganisha na faida ya Sh. bilioni 4.1 ya mwaka 2021.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NICOL, Erasto Ngamilaga, alitangaza mafanikio haya alipozungumza na mwandishi kwenye Maonesho ya Sabasaba, Dar es Salaam jana.

"Faida hiyo ni ongezeko la zaidi ya asilimia 51 na mapato ya kila hisa nayo yameongezeka kwa asilimia 42. Kwa hiyo, haya ni mapinduzi makubwa sana kwa kampuni yetu na wanahisa waendelee kutarajia makubwa zaidi kwa mwaka 2023," alisema.

Erasto alisema viongozi wa kampuni hiyo wameendelea kuwa na maono na mikakati madhubuti inayokwenda sambamba na uwekezaji wenye lengo la kuongeza mapato ya wanahisa wake.

Alisema takwimu za Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) zinaonesha kampuni ya NICOL inaendelea kufanya vizuri kwa kuwa hisa zake kwa sasa zinauzwa kwa Sh. 475 kwa hisa moja.

"Mwelekeo ni mzuri sana na kwa tunavyokwenda, muda si mrefu hisa zetu zitaanza kuuzwa kwa Sh. 1,000. Ndiyo maana tunawashauri wananchi wachangamkie hisa zetu kwani zina faida kubwa," alitamba.

"Kwa sasa uwekezaji wa kampuni yetu umefikia Sh. bilioni 130 na tumeamua kuja hapa kwenye Maonesho ya Sabasaba kuwapa fursa wanachama ambao hawakupata fursa ya kufika ofisini kwetu na kuchukua gawio lao kwa miaka mingi waje hapa watapata huduma nzuri sana," aliahidi.

Alisema kuwa tangu kampuni hiyo ilipoanza kutoa gawio mwaka 2017, ni miaka sita sasa kuna baadhi ya wanahisa ambao hawajapata gawio lao, hivyo kuwapo kwao Sabasaba ni sehemu ya kutengeneza urahisi kwa wanahisa hao kujaza fomu ili walipwe gawio lao.

# Dk. Tulia apitishwa urais IPU

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, amepitishwa na Mabunge ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kugombea nafasi ya Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

Uchaguzi unatarajiwa kufanyika Oktoba 27 mwaka huu huko Angola.

Mbunge wa Bunge la Afrika ya Kusini, Darren Bergman ndiye aliwasilisha hoja katika Bunge hilo wakati wa kikao cha 53 cha Jukwaa la Mabunge ya SADC kinachoendelea jijini Arusha na kuomba mabunge yote kumuunga mkono Dk. Tulia.

Alisema ametoa hoja ya kupitishwa Dk. Tulia kuwania nafasi hiyo kwa mujibu wa kanuni ya 26(4) ya utaratibu katika Bunge hilo.

Alisema amewasilisha hoja ya kupata mgombea mmoja kutoka SADC licha ya kuwapo wabunge wengine walioonesha nia kugombea nafasi hiyo kutoka Afrika.

Wagombea hao ni Catherine Hara wa Malawi, Jacob Fransis Mudenda wa Zimbabwe na Adji Diarra Kanoutee wa Senegal.

Bergman alisema ili kuonesha umoja katika kuwania nafasi hiyo, ni vyema kumpitisha Dk. Tulia kutokana na sifa alizonazo, kuwa mgombea wa SADC katika uchaguzi huo.

Hoja ya mbunge huyo kutoka Afrika Kusini, iliungwa mkono na mbunge kutoka Angola, Pedro Sebastiano na kueleza kuwa kwa muda mrefu nafasi hiyo imekuwa ikishikwa na wabunge wanaume, hivyo kumpitisha Dk. Tulia ambaye ni msomi na kijana kuwania nafasi hiyo kutaleta ushindi.

"Ninaunga mkono hoja hii na ninawaomba wabunge wenzangu tuunge mkono, ili kuonesha umoja na mshikamano ndani ya SADC, hasa kuwa na mgombea mwanamke na ni kijana," alisema.

Akizungumza baada ya kutolewa hoja hiyo, Rais wa Bunge la SADC, Roger Mancienne, alitoa fursa ya wabunge kuchangia hoja hiyo. Wabunge kutoka nchi za Zimbabwe, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Lesotho, Zambia, Eswatini, Namibia, Afrika Kusini na Mauritania walieleza kumuunga mkono Dk. Tulia.

Baada ya kupitishwa kuwania nafasi hiyo, Dk. Tulia aliwapongeza wabunge wote kwa kumpitisha, akisema heshima aliyopewa ni kubwa.

Dk. Tulia pia amepitishwa pia na Bunge la Afrika (PAP) na Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EALA) kuwania nafasi hiyo.

# TRA yasema Tanzania ina walipakodi wakubwa 700

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema ukuaji wa uchumi umeongeza walipakodi wakubwa kutoka 10 mwaka 2000 hadi zaidi ya 700 mwaka huu.

Kaimu Kamishna wa Walipakodi Wakubwa wa TRA, Kayobyo Majogoro, alibainisha hayo jana kwa waandishi wa habari alipotembelea Maonesho ya Sabasaba yanayoendelea mkoani Dar es Salaam.

Alisema walipakodi hao wakubwa wanachangia theluthi mbili ya makusanyo ya kodi zote za ndani na hivyo kuchangia ujenzi wa Taifa.

Kamishna Majogoro alisema kuwa katika Maonesho ya Sabasaba, wananchi wanapata huduma zote za TRA. Sheria ya kodi inawahusu wateja wadogo, wa kati na wakubwa.

"Kwa ujumla, utoaji wetu wa huduma ni wa viwango vinavyofanana. Sheria inayohusu walipakodi wakubwa ndio hiyo hiyo inayohusu walipakodi wadogo na wa kati. Kinachofanyika kwa walipakodi wakubwa ni kuweka dirisha maalum la kuwapa huduma," alisema Majogoro.

Alitoa wito kwa wananchi kufika katika banda la mamlaka hiyo kupata huduma na kwa wenye maoni au kero wafike ili watatuliwe changamoto zinazowakabili.

Kwa mujibu wa TRA, walipakodi wakubwa ni pamoja na benki kubwa za kibiashara, kampuni za mafuta na gesi, mifuko ya hifadhi ya jamii, kampuni za ujenzi na TRA yenyewe.



Mwakilishi kutoka ubalozi wa Sweden Tanzania, Annie Sturige (kushoto), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Uratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Haika Shayo, wakati wa ziara ya kukagua na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya mpango wa kunusuru kaya maskini nchini katika kijiji cha Itundwi, wilayani Kondoa mapema wiki hii. Kulia ni Maryam Ali Issa kutoka Tume ya Mipango Zanzibar. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wanafunzi, walimu washangaa baa zina umeme, shule haina

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Madilu ya wilayani Ludewa mkoani hapa, wamelalamikia kukosekana nishati ya umeme shuleni huko, wakidai kunachangia washindwe kujisomea usiku.

Katika mazungumzo na mwandishi juzi, wanafunzi hao walisema wanaumia kuona maeneo mengine zikiwamo nyumba za starehe kuna umeme ilhali shuleni kwao hawana nishati hiyo. Wanalazimika kutumia umeme wa jua ambao si wa uhakika.

Mmoja wa wanafunzi hao, Exavery Erick, alisema kukosekana kwa nishati hiyo shuleni ni tatizo kubwa kwa maendeleo yao kitaaluma.

"Suala hili linatuathiri kwa sababu unapokuwa unasoma ule mwanga ambao unatoka kwenye solar (umeme wa jua) unaumiza sana macho. Wanafunzi wengi wanaumwa macho, wanatumia miwani, kitu ambacho siyo kizuri.

"Hii ni changamoto kubwa. Tunakosa ari ya kujisomea kwa sababu ukiingia darasani unakutana na umeme wa jua ambao ukikaa saa moja, saa mbili au saa tatu unazima. Taa zikizima ndiyo basi tena, inabidi tukalale usiku. Shule inakuwa giza," alilalamika.

Erick aliiomba serikali kuwapatia nishati ya umeme kwa kuwa nguzo za umeme haziko mbali na shule yao.

Kiongozi wa wanafunzi shuleni huko, Musa Mwang'ombe, alisema suala hilo limekuwa changamoto kubwa shuleni. Serikali itatue kero hiyo ili wawe na uhakika wa kusoma wakati wowote.

Dada Mkuu shuleni, Magret Mlelwa, alisema changamoto ya umeme inasababisha wanafunzi kushindwa kusoma vizuri.

Mkuu wa shule hiyo, Michael Mwalongo, alisema changamoto ya kukosekana kwa umeme shuleni huko inatokana na huko nyuma wakati miundombinu inapitishwa eneo hilo lilirukwa.

"Tulipohoji kwanini eneo hili linarukwa, tuliambiwa kwamba utaletwa wa awamu ya pili. Awamu ya pili ilipofika ikawa hivyo hivyo, tukaendelea kupaza sauti kwa viongozi wa kata, wilaya.

"Ngazi ya mkoa hatujafika kwa sababu bado tunao viongozi huku. Tumefanya jitihada kuandika barua kwa TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) wilaya, tumeahidiwa lakini bado.

"Tunashangaa mtaani umeme upo, kwenye baa umeme upo lakini kwenye taasisi nyeti kama hii ya vijana ambao wanapikwa kuwa wasomi hakuna umeme. Wanafunzi wote wanakaa hosteli, nyakati za masika, jua linakuwa halipo (umeme wa jua). Kwa hiyo, wanashindwa kujisomea usiku.

"Mara nyingi taaluma inakuwa chini kulinganisha na shule zingine za jirani zenye umeme," alilalamika kiongozi huyo.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Michael Hadu, alikiri kuwapo changamoto hiyo shuleni huko na kunakosababisha shule kutofanya vizuri katika mitihani ya kitaifa.

"Mwaka jana ilikuwa kati ya shule tatu duni za Mkoa wa Njombe na tulipofuatilia programu ya KPI tumebaini kinachochangia zaidi ni ukosefu wa mwanga wa umeme na katika hili Mkuu wa Shule aliandika barua kwa Meneja wa TANESCO Wilaya ya Ludewa.

"Mimi mwenyewe nimefika naye kule wamechukua taarifa zetu, wakabainisha shule ambazo hazijapata umeme na mara kwa mara tumekuwa tukifuatilia wanatuambia wanaandaa bajeti," alisema Hadu.

Kiongozi huyo aliomba wahusika washughulikie changamoto hiyo kwa kuwa maendeleo ya taaluma shuleni huko yanarudi nyuma na walimu wanaopangwa kufundisha nao hawafurahishwi na hali hiyo.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Ludewa, Yusuph Sukwa, alisema Kata ya Madilu haipewi huduma na TANESCO, bali mwekezaji ambaye ni mzalishaji wa umeme Madope Hydro Power Company.

Mwandishi alipomtafuta Meneja wa Mradi wa Madope, Kulwa Masanja, alikiri kuwapo changamoto hiyo shuleni huko. Bajeti ya kupeleka umeme katika shule hiyo tayari imeshatengwa.



# Mwinyi aagiza balozi kuanzisha vituo kueneza lugha ya Kiswahili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezitaka balozi zote za Tanzania kuanzisha vituo vya lugha ya Kiswahili na utamaduni wake ili kuitangaza na kuieneza nje ya nchi.

Aliagiza hayo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya pili ya Siku ya Kiswahili Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Kambi ya Jeshi la Polisi Ziwani, mjini Unguja.

Alizipongeza baadhi ya balozi zilizofungua vituo vya kufundisha lugha ya Kiswahili, akizitaja ni za Korea ya Kusini, Italia, Falme za Kiarabu, Uholanzi, Ufaransa, Quba, Nigeria na Sudan.

"Ninatoa shukrani za pekee kwa Ubalozi wa Korea Kusini kwa kuanzisha mafunzo ya utamaduni wa Mswahili unaohusisha mambo tofauti ikiwamo vyakula, ngoma, mavazi na lugha. Ubalozi huu unastahili pongezi kwa kufanya vyema zaidi na ni wajibu kwa balozi zingine kuiga mafanikio haya," alisema.

Rais Mwinyi alisema kitendo cha Kiswahili kupewa hadhi na kuwekwa siku maalum ya kukiadhimisha, ni heshima kubwa ambayo imeipa nguvu lugha hiyo kutambulika duniani na ni ya kwanza kwa Afrika kupewa siku maalum.

Alisema kufanyika kwa sherehe hizo ni njia mojawapo ya kutoa hamasa katika kueneza Kiswahili duniani, hivyo ni lazima kuhakikisha maadhimisho hayo yanaendelezwa kwa sababu yanaimarisha na kuhamasisha matumizi ya lugha hiyo.

Kiongozi huyo pia aliyapongeza mabaraza ya Kiswahili na taasisi zinazosimamia na kuendeleaza lugha hiyo kwa kuungana na balozi mbalimbali katika jitihada za kukiendeleza.

"Tunafahamu na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) katika kukieneza Kiswahili ikiwamo kusambaza kamusi na vitabu katika balozi mbalimbali kwa ajili ya kutoa taaluma juu ya mbinu za ufundishaji wa Kiswahili," alisema.

Dk. Mwinyi pia aliwataka wataalamu wa lugha ya Kiswahili kutumia fursa hiyo ya mahitaji ya vitabu na walimu wa lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani.

Alipongeza Wizara ya Habari, Vijana na Utamaduni Zanzibar na Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na kamati kwa ubunifu kujumuisha mambo mbalimbali ili kuyaongezea hamasa maadhimisho hayo ya Siku ya Kiswahili Duniani.

"Tujitahidi kufuatilia na kuzitumia fursa za Kiswahili zilizomo ndani na nje ya nchi yetu, kwa sababu mahitaji ya lugha ya Kiswahili duniani yanaendelea kuongezeka kila siku," alisema.

Dk. Mwinyi alisema kwa sasa fursa zitafunguka katika kupata mahitaji ya walimu kwa balozi kufundisha Kiswahili na kutoa rai kwa pande zote za Muungano kushirikiana kikamilifu katika kutoa mafunzo nje ya nchi.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema wanaendelea kusimamia sera na sheria zilizowekwa katika mabaraza ya Kiswahili yenye lengo la kukikuza, kukieneza Kiswahili na kuwa bidhaa ili kuleta pato katika nchi.

Alipongeza ushirikiano uliofikiwa kati ya viongozi waliokabidhiwa majukumu ya kutangaza Kiswahili. Umepata mafanikio makubwa.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Pindi Chana, alisema kwa sasa Kiswahili kinatumiwa na zaidi ya watu milioni 500 duniani. Kinaenea kwa haraka duniani.

Alisema kasi ya kukieneza inaendelea katika ofisi za balozi mbalimbali duniani kupitia BAKITA na BAKIZA.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Elimu (UNESCO), Mishel Toto aliipongeza serikali kwa jitihada zake katika kukitangaza Kiswahili katika pande zote za duniani.

Alisema, hivi sasa umaarufu wake umeenea katika Bara la Ulaya ikiwamo kufundishwa katika vyuo vikuu, hatua ambayo ameitaja imesaidia kukieneza na kutoa ajira kwa vijana wanaofundisha.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi (wa pili kushoto), akimpongeza mwajiri ambaye ni Mwanachama wa WCF, Isani Longo, kutoka kampuni ya Elfatel Enterprises Ltd ya wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma aliyefika kwenye banda la WCF kupata elimu ya fidia kwa wafanyakazi katika maonyesho ya 47 ya biashara ya kimataifa Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEA), Juma Buruhani Mohammed. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sekta ya mifugo yaundiwa mkakati kuongeza ajira na kukuza uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema serikali imeweka malengo kuhakikisha mchango wa sekta ya mifugo unaongezeka katika Pato la Taifa kufikia asilimia 30 na kutoa ajira kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na Balozi Mdogo wa Umoja wa Falme za Kiarabu, Sheikh Saleh Ahmed Alhemeir, katika kujenga mikakati ya kuimarisha uhusiano wa pande mbili katika ufugaji wa kisasa.

Waziri huyo alisema sekta ya mifugo haijaleta tija kwa wananchi wengi ikiwamo wafugaji wazalendo katika kufunga kwa kutumia mbinu za kisasa zenye tija.

Alisema, hivi sasa mahitaji ya nyama ya kuku ni makubwa katika hoteli za kitalii pamoja na mayai na maziwa ambapo uzalishaji wake bado ni mdogo.

Shamata aliuomba umoja huo kuipatia Zanzibar mtambo wa uzalishaji wa gesi kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa.

"Moja ya mahitaji yetu makubwa katika sekta ya ufugaji ni mbinu za kisasa ambazo zitatuwezesha wafugaji wetu kupata kipato kikubwa na kutosheleza soko la utalii ambalo mahitaji yake ni makubwa," alisema.

Balozi Sheikh Alhemeir alisema nchi yake ipo tayari kusaidia sekta ya ufugaji kwa kuwa wamepiga hatua kubwa katika uzalishaji wa mifugo.

Alisema nchi yake inatarajia kuleta wataalamu ambao watatoa elimu na mbinu za ujuzi katika ufugaji wa kisasa na kukidhi mahitaji ya soko la ndani. Balozi huyo alisema ufugaji wa kisasa wenye kutumia mbinu, ndiyo utakaowakomboa wakulima nchini na kufanikiwa kuwainua kiuchumi na uwekezaji katika sekta ya ufugaji.

"Nimepokea ombi la kusaidia maendeleo ya sekta ya ufugaji kwa sababu nimeona yapo mahitaji makubwa ya soko la nyama pamoja na maziwa kuimarika kwa sekta ya utalii," alisema.

Balozi huyo alisema kuwapo kwa Ofisi ya Ubalozi Mdogo wa Umoja wa Falme za Kiarabu ni nafasi nyingine ya kujenga ushirikiano katika sekta mbalimbali, ikiwamo uchumi na maendeleo.

## Balozi Ali Karume aishauri CCM uteuzi uzingatie uzoefu kiuongozi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MTOTO wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Balozi mstaafu Ali Karume, amekishauri Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuepuka kufanya alichokiita makosa ya uteuzi kwa wanachama wake ambao hawajawahi kushika nafasi za chini za kisiasa na kiserikali kupewa nyadhifa za juu.

Balozi Ali ameonya kuwa uteuzi wa aina hiyo unasababishia chama hicho kupata viongozi aliowaita dhaifu, wasiojua maana ya siasa, uongozi na utawala.

Alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake Maisara kuhusu Sikukuu ya Sabasaba na historia ya kuunganishwa vyama vya TANU na Afro Shirazy Part na kuzaliwa CCM mwaka 1977.

Balozi Ali alisema kimsingi wagombea au wanaoshika nafasi za kisiasa na kiserikali lazima wawe wanachama wenye sifa ili kupata viongozi bora kwa manufaa chama na serikali.

Alisema wapo baadhi ya viongozi ambao wanajulikana hawakuwahi kuongoza hata ngazi ya kata au tawi.

"Chama chetu ni kikubwa kinachoaminiwa na wananchi. Tuna wanachama wengi wenye sifa zinazostahili. Wanapoachwa na kuteuliwa wasio na sifa ya uongozi, badala ya kusonga mbele kinajikuta kikirudi nyuma," alionya Balozi Karume.

Balozi huyo alisema utamaduni wa kiongozi mmoja tu kuwa na sauti au uamuzi kwa jambo analolitaka yeye lifanyike, matokeo yake ni kupata kiongozi dikteta ambaye hatokani na historia ya chama.

"Hatuna upungufu wa viongozi ambao hawakupitia ngazi za chipukizi au jumuiya za chama. Anapoteuliwa kiongozi mwanagenzi ashike nafasi nyeti, hatomudu kuleta mabadiliko yanayotarajiwa," alisisitiza.

Kuhusu maendeleo ya siasa visiwani humo, Balozi Ali alisema vyama vilivyoungana mwaka 1977 ni TANU na ASP kitaifa, lakini kwa Zanzibar anaona CCM haionyeshi umoja madhubuti bali viongozi wachache wanaohodhi uamuzi ya chama.

Akijibu madai kwamba Hayati Mzee Abeid Amani Karume alipewa urais na ASP bila kushiriki mapinduzi, Balozi Ali alisema chama kilichofanya mapinduzi ni ASP ambacho Rais wake alikuwa Mzee Karume.

"Kwa kuwa mapinduzi yalifanywa na ASP, yaliongozwa na Rais wake akiwa kiongozi mkuu, hata kama vijana wake ingetokea kushindwa kupindua serikali iliyokuwapo madarakani mshitakiwa namba moja angelikuwa Rais wa ASP," alisema.



YOUNG LUNYA
UKURASA 13



# WAMEPAGAWA
# WAMEONEKANA WASHAMBA PIA

DUNIA ni kama imesimama baada ya kampuni ya kutangaza ujio wa app mpya iitwayo Instagram threads, ambapo tangu kuanza kazi watu kama vile wamepagawa kutokana na utendaji wake wa kazi.

Mtandao wa Threads ambao upo kama ilivyo Twitter na Facebook , ulitambulishwa juzi na zaidi ya watumiaji milioni 30 walijiunga haraka.

Kundi la wasanii wa fani mbalimbali ambao hawakufurahishwa na Twitter, walionekna kushangilia zaidi na wengine wamejikuta wakishangaa kutokana na baadhi ya vitu kuwa vigumu.

Hapa nchini wasanii mbalimbali na watu maarufu walijiunga haraka katika mtandao huo na kuandika jumbe tofauti zinaozoonyesha furaha yao.

Uzinduzi wa threads unakuja baada ya mmiliki wa Twitter Elon Musk kununua Twitter na kuweka vipengele vingi vigumu kwa watumiaji wake.

Threads, inafanya kazi pamoja na Instagram japo iko kivyake, ukipakua lazima unganishe na akaunti yako ya Instagram hivyo wafuasi na jina la mtumiaji unaenda nao kwenye app hiyo mpya.

Mwanamuziki nyota Diamond Platnumz, mara baada ya kujiunga alionekana kushangaa zaidi pale alipoandika kwamba hakuona sehemu ya kuandika ujumbe binafsi.

Akiweka picha ambayo anaonekana akicheka aliandika "Msioweza kwenda DM kwenye Thread nawasalimia,"

Ali Kiba kwa upande wake ameanza kwa kuweka picha akionekna yeye na watoto wake wawili wakifurahi.

Naye Zuchu hakutaka kuwa mbali na mtandao huo, mara alipojiunga aliwasalimia mashabiki zake.

Nandy aliupokea mtandao huo akiwa eneo la sokoni na kuandika "Jamani niko sokoni ila bado nawaangalia mnaonifollow nikirudi nitawakubali,"

Msanii nyota wa filamu, Wema Sepetu, ameonekana kufurahia zaidi baada ya kueleza kwamba akiwa Threads anajikuta kama yuko kwenye kikao na rafiki zake.

"Hi Wapenzi wangu, huku ni pambe. Mhh! Naona huku kama nazidiwa kuchati jinsi ujumbe unavyomiminika halooo," ameandika.

BASI SAWA

## Will Paul utawapata wapi wenye nazo?



MKALI wa muziki wa Injili na nyimbo zingine, Wilson Radido almaarufu kama Willy Paul, ametoa ushauri wa bure kwa wanaume, akiwataka kujiepusha kujihusisha na wanawake ambao hawana pesa.

Will Paul amesema wanawake ambao hawana hela wanaweza kushika mimba kwa urahisi wanaposhiriki tendo la ndoa tofauti na wenye nazo kwa kuwa wanataka kuwa na mtambo wa kuzalisha pesa.

"Kaa mbali na wanawake ambao hawana hela, wanawake hawa wana uwezo wa kushika mimba kwa haraka sana."

## Chameleone bado hali tete

HALI ya mwanamuziki mahiri kutoka Uganda Jose Chameleone, inaelezewa kuwa mbaya baada ya kukabiliwa na tatizo la tumbo ambalo linamsababishia maumivu makali.

Baba mzazi wa mwimbaji huyo, Gerald Mayanja amethibitisha kuwa mtoto wake anaugua ugonjwa huo tangu ahamishie makazi yake nchini Marekani.

"Chameleone amekuwa mgonjwa katika miezi iliyopita. Alipohamia Amerika, ugonjwa ulizidi kuwa mbaya. Sasa ni mgonjwa sana, yuko kwenye kitanda chake cha wagonjwa. Amekuwa akipata matatizo ya tumbo ila kwa sasa anapokea matibabu," Mzee Mayanja ameiambia Bukedde Tv.





# MWENYE UWEZO ATEGUE

NINI kitatokea baada ya wanamuziki wawili mastaa kutoka Afrika mashariki, Diamond Platnumz na Koffi Olomide, kujifungia studio kwa ajili ya kukamilisha kibao chao cha pili?

Swali hilo limekuwa likiwaumiza mashabiki wengi wa muziki nchini baada ya wasanii hao kuonekana pamoja kukamilisha ngoma yao mpya ambayo bado haijafahamika.

Olomide, ambaye anatoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, yuko nchini kama mgeni wa Diamond kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo ambayo inaonekana itakuwa moto wa kuotea mbali baada ya nyimbo yao ya pamoja 'Waah' ya 2020 kufanya vizuri.





# Huyu hapa Young Lunya

RAPA anayefanya vizuri katika muziki, Young Lunya, jana ametambulisha singo yake kali ambayo ameiita Freestyle Session ya tano.

Katika ngoma hiyo ameionyesha ukali wake wa mistari ambayo ndani yake ameelezea maisha ya mtaani ambayo amekuwa nayo kwa muda mrefu.

Young Lunya, ametumia dakika tano kukamilisha wimbo huo ambao umepokelewa vizuri na mashabiki wa Hip hop hapa nchini.

# BONGO FLEVA KATIKATI YA MWAKA

**Na Adam Fungamwango**

TAYARI mwaka 2023 umegawanyika, kwani umeingia mwezi Julai ambao kiswahili unaitwa wa saba. Kumaliza nusu ya mwanzo wa mwaka, wasanii mbalimbali hawakuwa nyuma kutoa ngoma mwezi wa sita.

Mwezi Juni ulikuwa na pilikapilika za wasanii kupishana studio kurekodi nyimbo, kila mmoja akitaka kutoa wimbo wake kumalizia nusu mwaka.

Hizi ni baadhi ya ngoma zilizorekodiwa mwezi Juni na kuweka kumbukumbu kuwa zilitoka nusu ya mwaka 2023.

**Nakupenda-Rayvanny**

Rayvanny ametoa ngoma hii Juni 30, mwisho kabisa wa mwezi huo. Wala haikuwa bahati mbaya, alichotaka ni kuona anamaliza nusu mwaka na kuingia kipande cha pili cha miezi sita mingine akiwa na ngoma nyingine.

Akaimba kwenye lugha tatu, ambazo ni Kingereza, Kinyarwanda na Kiswahili. Ni wimbo wa mapenzi kama zilivyo nyingi za bongo fleva.

**Tajiri-Lavalava**

Ilikuwa ni siku hiyohiyo, msanii Lavalava naye alipotoa ngoma yake, yeye akaiita 'Tajiri.' Inaeleza jinsi mtu mwenye uwezo au tajiri alivyokuwa muhimu kwa watu wengine.

"Nilikupigia simu, nikatia timu mjengoni sijakupata, akili ikaingia wazimu nitakuje bata, wewe ni mtu muhimu, nikiwa nawe najipata." Ni moja kati ya mistari kwenye ngoma hiyo.

**Tiririka-Yammi**

Binti anayefanya vizuri sana kwenye tasnia ya muziki wa bongo fleva kwa sasa. Anaitwa Yammi ambaye ukitizama ngoma zake na video, anatishia umalkia wa wasanii wengine wa kike nyota nchini. Sifa yake anajua kuimba na kucheza pia.

Video ya ngoma yake mpya 'Tiririka' imetoka Juni 27. "Mapenzi yamenibadilisha, siku hizi sinaga ubabe, nimeshakuwa guta, acheni moyoni niyabebe, mimi kuku wako ukitaka mayai niyatage, sema, na ukina ujiga, we nisubiri usikibwage.

Mapenzi siyo mchezo wa ngumi nipige na khanga au ukuni hata ukinifinyafinya haiumi, naona raha naisoma namba, huu mchezo gani mbona wa kihuni, hata ukifinyafinya haiumi." Yammi analalamika kwenye songi hilo.



**Sitaki-Mbosso**

Mbosso, mmoja wa wasanii wa bongo fleva ambaye hata kukiwa na mashindano ya kutoa ngoma kila wiki, anaweza kufanya hivyo na zote zikawa nzuri.

Baada ya ile 'Amepotea', katoa nyingine inaitwa 'Sitaki.' Huyo ndiyo Mbosso, haitaji maelezo marefu zaidi ya kusikiliza ngoma zake.

**Yesa-Chino Kidd**

Kwenye ngoma hii ameshirikisha Jaivah na Marioo. Inaitwa 'Yesa'. Ni moja ya ngoma iliyochamka saidi na kuchezeka.

"Shauri zao, kimpango wao, kwani si hatuli kwao? Na mwaka huu tutapiga 'baby' zao." Maneno haya, yamo kwenye ngoma hiyo iliyotoka Juni 25.

FILAMU

# Changudoa: Uchangudoa hadi mke mwema

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine binadamu anapitia kwenye mazingira magumu na tata hadi kuwa mtu mwema.

Kwa wale anaokwenda kwenye makanisa, ni mashuhuda kwa watu wanaotoa ushuhuda kuwa walikuwa wachawi, majambazi, au wala rushwa, lakini baadaye wanatubu, wanamrudia Mungu na kuwa watu wema.

Hiki ndicho kisa kilichomo kwenye filamu hii itwayo 'Changudoa.'

Filamu hii imechezwa na wasanii kina Nassor Ndambwe, Flora Mvungi, Abdul Mhema na wengine wengi.

Inaanza kwa kumuonyesha kuwa Flora ni msichana ambaye kazi yake ni kuuza mwili.

Anafanya kazi ya ukahaba, ndiyo inayomfanya kupata mahitaji yake ya kila siku.

Filamu inamuonyesha kuwa yupo na mteja kwenye nyumba ya kulala wageni.

Lakini anafanya kitu cha ajabu, baada ya kuamka huku mwenzake akiwa amelala na kwenda kumkomba kila kitu na kutimka, wakati mteja wake akiwa kwenye usingizi fofofo.

Anapoamka hamkuti mwenzake kitandani na anashangaa kuona nguo zake zimetupwa chini na hatimaye kugundua kuwa amelizwa kila kitu na changudoa aliyemchukua.

Siku nyingine anampata mwanaume mwingine aitwaye Abdul. Wakiwa kwenye nyumba ya kulala wageni anavamia mtu mmoja anayejulikana kwa jina la Ndambwe ambaye anatoa bastola kumuonyesha Flora, akimwambia amlipe pesa zake alizomwibia, sivyo atammaliza. Ilimuogopesha Abdul na kuamua kuchukua yeye jukumu la kulipa pesa hizo.

Abdul anaonekana kumpenda sana Flora kiasi cha kumwambia kuwa anahitaji kumuoa.

Kutokana na hilo, anaamua kumpeleka nyumbani kwake. Wanapofika wanakutaka na Ndambwe ambaye analianzisha vurugu.

Baba mwenye nyumba anatoka baada ya kuona nje kuna ugomvi, lakini anakutana na mpangaji wake Abdul pamoja na Flora ambaye ameshawahi kumchukua na kwenda naye kufanya naye mapenzi gesti.

Sasa ugomvi unakuwa mkubwa zaidi kiasi cha Flora, kuwachoropoka na kutimua mbio kuepuka kupigwa.

Anapofika nyumbani anawapigia simu shoga zake kuwaeleza yaliyompata na jambo hilo lilimwathiri kisaikolojia kiasi cha kuamua kuachana na kazi hiyo.



Akaamua kufanya kazi ya kuuza maandazi, lakini kwa sababu hajaizoea, alijikuta sehemu kubwa ya maandazi akirudi nayo nyumbani na kuyatafuna yeye na shoga zake.

Alikaa na kifikiri, akili ikamtuma kurudia tena kazi yake ya uchangudoa. Huko tena alikutana na Abdul. Flora alitaka kuimbia akidhani atapigwa, lakini jamaa anamwambia hakuna na nia hiyo, ila azma yake iko pale pale ya kumuoa.

Flora alikataa kwa madai hana hadhi hiyo. Abdul alimbembeleza na kumwambia kuwa kitu anachotakiwa kufanya ni kuanza ukurasa mpya akishakuwa mke wa mtu.

Flora alitafakari kazi ya uchangudoa na kuona tayari imeshamletea matatizo, huku kazi ya kuuza maandazi ikiwa hailipi, upande wa pili kuna mtu anamtaka awe mkewe, kitu ambacho ni nadra sana.

Anakubali kuolewa na kubadilisha tabia. Abdul amuoa na kumuondoa sehemu ambayo amezoeleka na kwenda kuishi naye mbali na hapo. Akawa mke mwema.



# Jung-Jae aikana Squid Game 2

MSANII wa filamu maarufu ya Squid Game, Lee jung-Jae, amekanusha kushiriki kuigiza katika mwendelezo wa filamu hiyo kwa awamu ya pili.

Jung-Jae ametoa kauli hiyo baada ya kampuni ya Netflix, kutoa tangazo la kuanza mchakato wa kucheza filamu hiyo awamu ya pili na kuwashirikisha mastaa wa Korea Kusini akiwamo Jung-Jae mwenyewe, Wi Ha-joon, Gong Yoo na Lee Byung-hun.

'Tungependa kueleza msimamo wetu kuhusiana na ripoti kuhusu mwigizaji Lee Jung Jae kuhusika katika uigizaji wa Squid Game 2. Baadhi ya ripoti zinazodai mwigizaji Lee Jung Jae alihusika katika uigizaji wa Squid Game 2 si za kweli," imesema taarifa hiyo.



## Micki Minaj naye!

RAPA mwenye vituko vingi, Nicki Minaj, amebadilisha siku ya kutambulisha albam yake mpya ambayo alitarajia kuitoa Oktoba 29, mwaka huu na sasa ameipeleka mbele katika siku isiyojulikana.

"Kwa sababu ya habari za kusisimua ambazo nitashiriki nawe baadaye, nimebadilisha tarehe ya kutambulisha albam. Niamini, itakuwa nachelewa kidogo, lakini kwa kuwa ninahamisha tarehe kidogo tu, ningependa kuwapa watu vionjo kidogo vya albamu ili nisilazimike kusemwa sana," amebadilika kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Hivi karibuni mwanamuziki huyo alionekana kwenye wimbo mpya wa Young Thug 'Money' pamoja na Juice WRLD na akajiunga na Ice Spice kwa wimbo unaokwenda kwa jina la 'Barbie World'.

## Omba Mungu isiwe kweli


MAHAKAMA inasubiriwa kuamua kama kuna ushahidi wa kutosha wa kufunguliwa mashtaka ya uhalifu dhidi ya Travis Scott au watu wengine walioandaa tamasha la Astroworld, lililosababisha vifo vya watu 10 mwaka 2021.

Wakili Kent Schaffer anayemwakilisha Travis ana uhakika kwamba hakuna mashtaka yatakayofunguliwa.

"Hakuna kitu ambacho Travis alifanya au kushindwa kufanya kinacholingana na kanuni za uhalifu za Texas," amesema Schaffer.

Uchunguzi unafanyika kuhusu msongamano wa watu kwenye tamasha la Astroworld mjini Houston, ambapo maelfu ya watu walijeruhiwa kutokana na mkanyagano.





## Kiibii usikimbie kivuli chako

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Kiibii Mayana, amesema hawezi kusimulia kuhusu kifo chake feki kilichotokea miaka ya nyuma.

Katika mahojiano yake na Adesope Olajide kwenye Afrobeats Podcast, Skiibii amefafanua kuwa kashfa ya kifo feki iliyotokea 2015, hawezi kukataa wala kukubali kutokana na kukabiliwa na matukio ya kuzimia mara mbili.


" Sipendi kuongelea, kila mtu anaweza. sema wanachotaka kusema, kwa sababu nilikuwa na matatizo ya kuzimia mara mbili nikiwa safarini," amesema Kiibii.

## Wanaomsumbua Bella waache

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria, Bella amefichua kuwa hajawahi na hatashiriki mapenzi hadi hapo atakapofunga ndoa.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Bella ameeleza kwamba wanaume wanaoendelea kumsumbua wanatakiwa kusitisha maombi yao kwani hawezi kufanya mapenzi kabla ya kuolewa.

"Kitu kimoja cha kuzingatia katika mafunzo ya nyumbani ni kuhakikisha usifanye ngono kabla ya ndoa, mimi nazingatia sana," ameandika na kuibua mjadala katika mitandao ya kijamii.





# Polisi adaiwa kuua kijana kwa kumpiga risasi tatu barabarani

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ASKARI Polisi wa kituo kilichopo karibu na Gereza la Kisongo mkoani Arusha aliyetajwa kwa jina moja la Eliwaha, anadaiwa kumuua kwa kumpiga risasi tatu, Daud Sindio, mkazi wa Oloresho, Kata ya Olasiti, wakati akijaribu kumsihi askari huyo kuiachia mifugo aliyokuwa ameikamata.

Jijini Arusha jana, Diwani wa Olasiti, Alex Martin, alidai tukio hilo lilitokea juzi saa saba mchana, maeneo ya Uwanja wa Ndege Kisongo jijini. Kijana huyo alifariki dunia alipokuwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru).

Diwani alisema alipata taarifa kuhusu tukio hilo na kufika eneo la tukio. Alikuta damu nyingi zikiwa zimetapakaa. Kijana anayedaiwa kupigwa risasi hakuwapo eneo la tukio.

"Nilipofika eneo la tukio niliongea na mashuhuda wakiwamo vijana wawili waliokamatiwa mifugo yao, ambao walinieleza kuwa mara ya kwanza askari huyo alimpiga mwenzao risasi pajani na kuanguka chini na kisha alimsogelea na kumpiga risasi zingine mbili akiwa chini na baadaye alimburuza na kumpakia katika gari la polisi, walilokuja nalo na kuondoka naye," alidai.

Diwani huyo alisema kuwa baada ya maelezo ya mashuhuda hao, aliamua kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa na kumkuta kijana huyo akiwa katika hali mbaya kiafya. Baadaye usiku wa kuamkia jana, alifariki dunia.

Alidai kuwa askari huyo alifika eneo la tukio baada ya kupata taarifa kuhusu kuwapo mifugo iliyoingizwa katika eneo lisiloruhusiwa kwa malisho.

Kiongozi huyo aliendelea kudai kuwa askari huyo aliikamata mifugo hiyo na wachungaji wawili na kuanza kuiswaga kuipeleka alikojua mwenywe, lakini ghafla alitokea kijana Sindio akiwa na pikipiki na alipowaona vijana hao aliwatambua na kuamua kwenda kuongea na askari huyo, ili kujua kilichotokea na kumsihi askari huyo awaachie na mifugo yao.

"Lakini askari huyo alionekana kuwa mkali ndipo marehemu alipoamua kuondoka na kwenda kuchukua pikipiki yake ili aendelee na safari yake, lakini kabla hajafika mbali askari huyo alichomoa silaha yake na kumpiga risasi moja kwenye mguu na kijana kuanguka chini. Baadaye alimsogelea na kumfyatulia risasi zingine mbili eneo la mapajani," alidai.

Aliendelea kudai kuwa askari huyo aliamua kumburuza majeruhi huyo hadi alipokuwa ameacha gari na kumpakia na kuondoka naye na baadaye kumpeleka katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa alikofariki dunia baadaye.

Diwani huyo alilitaja ni tukio hilo la pili kwa askari huyo kudaiwa kufanya uhalifu katika kata hiyo ya Olasiti. Alishawahi kutuhumiwa kutisha wananchi kwa silaha na wananchi walijikusanya na kutaka kumdhuru, na kama si yeye (diwani) kuingilia kati kumnusuru askari hiyo, angeuawa.

"Lakini cha kushangaza askari huyo amerudia tena kufanya vitu vya aina hii. Hivyo, ninaomba Jeshi la Polisi kutotumia nguvu na mabavu kwa raia wake pasipo sababu," alisema. Baba mdogo wa marehemu, Richard Mollel, akizungumza na Nipashe jana katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha, alidai ndugu yao huyo alipigwa risasi na askari huyo majira ya mchana juzi. Alipokwenda eneo la tukio, ndugu yao alikuwa ameshachukuliwa na kupelekwa hosptalini.

"Tulipofika Mount Meru tulimkuta mtoto wetu akiwa na hali mbaya. Baada ya muda mfupi alihamishiwa ICU (chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum)," alidai.

Kwa mujibu wa Mollel, walijulishwa na madktari kuwa inahitajika damu kwa ajili ya kumwongeza mtoto wao huyo.

Alidai kuwa ndugu yao hakuwahi kujihusisha na vitendo vyovyote vya kihalifu. Wamesikitishwa na kitendo cha kupigwa risasi bila hatia.

"Simtetei mtoto wetu. Hata kama alikuwa na makosa, alitakiwa kukamatwa kama mwalifu na kufikishwa mbele ya sheria, siyo kupigwa risasi na ikitokea amefariki dunia, sisi familia hatutazika mwili wake badala yake utakwenda kuzikwa nyumbani kwa huyo askari Eliwaha," alidai.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Jonh Mongela, alipoulizwa kuhusu tukio hilo alithibitisha kuwa na taarifa hizo, anafuatilia na atatoa ufafanuzi baadaye.

Mwandishi alipomtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Justine Masejo, alikiri kuwapo tukio hilo. Wanaendelea na uchunguzi.

Mwili wa kijana huyo umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha kwa ajili ya uchunguzi.

Ni tukio ambalo linashabihiana na lililotokea mkoani Simiyu Juni 11 mwaka huu la kijana Mandela Petro (26), mkazi wa Mtaa wa Zambia, Kata ya Malampaka wilayani Maswa, anayedaiwa kuuawa na askari polisi.

Inadaiwa kuwa kifo cha kijana huyo kilisababishwa na kipigo toka kwa askari polisi wawili kwa tuhuma za wizi. Kumeundwa timu ya uchunguzi wa tukio hilo pasi na kuelezwa wajumbe wake na hata muda wa kukamilika kwa uchunguzi huo.



Baadhi ya wageni waalikwa wakifuatilia uzinduzi wa huduma ya NBC Connect inayowezesha kufanya miamala kwa urahisi kwa njia ya kidigitali, jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Halmashauri wakwama tena

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

UCHAGUZI wa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, umekwama kwa mara ya tatu, kutokana na madai kwamba madiwani wameususa.

Mkwamo huo unaelezwa kuanzia katika kikao cha ndani cha Chama Cha Mapinduzi (CCM), kukiwa na madai kwamba Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, na baadhi ya madiwani, wameugomea, wakipinga kukatwa majina ya madiwani wanne walioomba nafasi hiyo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Simanjiro, Amos Shimba, alithibitishwa kutofanyika kwa uchaguzi huo wa kumpata Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo kupitia chama hicho.

"Ni kweli uchaguzi wa kumpata Makamu umevurugika na haujafanyika, ila tumeshatuma taarifa ngazi ya juu kwa hatua zaidi. Subirini mtapatiwa majibu," alisema Shimba.

Inaelezwa kuwa Kamati ya Siasa ya Mkoa na Wilaya zilipitisha majina matatu ambayo ni ya Albert Msole (Ngorika), Lucas Zacharia (Endiamtu) na Kaleiya Mollel (Msitu wa Tembo) kupigiwa kura kuwania nafasi hiyo.

**"Ni kweli uchaguzi wa kumpata Makamu umevurugika na haujafanyika, ila tumeshatuma taarifa ngazi ya juu kwa hatua zaidi. Subirini mtapatiwa majibu," alisema Shimba.**

# NGO 440 zakutana kujadili kilio cha kodi zinazotozwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KILIO cha tozo ya kodi ya mwaka ya asilimia 30 inayotokana na mavuno ya mapato ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), kimezikutanisha pamoja asasi za kiraia zaidi ya 400 mkoani Kilimanjaro, kupaza sauti zikitaka serikali kuiondoa.

Wakati wanapaza sauti zao, serikali nayo imezipongeza asasi za kiraia 110, kati ya 443 za Kilimanjaro kwa kutekeleza miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 6.1.

Mratibu wa Taifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Wakili Onesmo Ole Ngurumwa, wakati anawasilisha mada kuhusu changamoto ya kodi kwa NGO, elimu ya kodi na matumizi ya mfumo wa kodi kimtandao, alisema hawaoni sababu ya kulipishwa kodi zisizostahiki.

Ole Ngurumwa alikuwa akizungumza jana kwenye Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Mkoa wa Kilimanjaro, lililoratibiwa na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO).

"Ziko kodi za kawaida, tunaweza tukalipa lakini zingine zile ambazo tunapigwa, kwa mfano ile ya kodi ya mwaka ya asilimia 30 ya mapato, sisi hatuna mapato.

"Sisi tuna ruzuku, na ruzuku siyo ya mtu binafsi ni ya kutoa huduma. Sasa ruzuku yangu ambayo inatumika mwaka kesho, ukiipiga asilimia 30 maana yake umeenda kutumia hela ya miradi.

"Ndiyo maana tumeona tukae vizuri na ndugu zetu wa TRA (Mamlaka ya Mapato) pamoja na serikali ili tuweze kuona ni namna gani tutaboresha sheria za kodi," alisema.

Kwa mujibu wa Wakili Ole Ngurumwa, kila unapopita asasi za kiraia wanalia, ombi lao kubwa ni kupata misamaha ya kodi hiyo inayolalamikiwa.

Akieleza dhamira ya jukwaa hilo kukutana, Mwakilishi wa NaCoNGO Mkoa wa Kilimanjaro, Asifiwe Mallya, alisema wamekutana ili kujadili kwa pamoja mafanikio na changamoto zinazowakabili katika sekta ya NGO.

"Lakini pia tumekuja kukumbushana taratibu na miongozo ikiwa ni pamoja na sheria ya uendeshaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali iliyowekwa kwa ajili ya usimamizi na uratibu wa mashirika haya. "Tunajengewa uwezo kuhusu elimu ya kodi, matumizi ya mfumo wa kimtandao na sheria za kuzuia ufadhili wa ugaidi na utakatishaji fedha," alisema.

Kwa mujibu wa Asifiwe, wanaharakati kutoka mashirika hayo, pamoja na mambo mengine, wanajadili mmonyoko wa maadili ambao linaikumba na kuitishia nchi kwa sasa.

Katika jukwaa hilo, Msajili Msaidizi wa NGO kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, Jesca Nyaki, alisema mkoa huo hadi sasa umesajili mashirika 443, lakini yaliyowasilisha taarifa za fedha na utekelezaji miradi yao kwa mwaka 2022 ni 110 pekee.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOKWENDA...

# Michael Jackson wa Bongo, Black Moses walivyoitendea haki disco

## •Kokoliko, Jobiso, Digadiga wakapagawisha mashabiki

Na Adam Fungamwango

MWANZONI mwa miaka ya 1990 kulitokea mapinduzi makubwa ya muziki Tanzania hasa kwa upande wa muziki wa disco.

Siyo kwamba muziki huo haukuwepo zamani la hasha, bali lilikuwepo tangu enzi la kumbi za Mbowe Hotels, YMCA, Rungwe Oceanic, Silver Sands, Msasani Club na zingine nyingi miaka ya 1980. Na hata mikoani nako kulikuwa na kumbi nyingi maarufu miaka hiyo.

Lakini ilipofika mwanzoni mwa miaka ya 1990, kulitokea mabadiliko au mapinduzi makubwa ya muziki huo, kwani ilitoka kwa baadhi ya watu kucheza muziki kama starehe ya kuanza kuwa kazi kamili.

Na hii ilisababishwa na televisheni kuanza kuingia nchini. Zilipoanza kuingia nchini, japo zilikuwa chache, lakini baadhi ya vijana walianza kupata bahati ya kuwatazama wanamuziki maarufu wa nje ya nchi akina Michael Jackson na wenzake, lakini pamoja na wanamuziki wa Zaire kwa sasa ni Congo DR.

Vijana wengi wakajifunza mitindo mbalimbali ya uchezaji wa muziki huo na kuwa mahiri mno, kiasi cha kuanza wengine kujiamini na kuanza kufanya kazi ya kuburudisha watu kwenye kumbi mbalimbali za burudani.

Hii ilivutia wengi na kuanza kuwakodi kwenye sherehe mbalimbali za harusi, hafla ya kiserikali na nyinginezo.

Ikaenda mbali zaidi kikaundwa mpaka chama cha wachezaji disco Tanzania, ambacho nacho kilianza kuandaa hata matamasha na mashindano ya disco ambayo yalitokea kuwa maarufu mno nchini na kuwafanya vijana hao mbali na kuishi kwa kipato cha kucheza muziki huo, pia kuwa maarufu sana nchini.

Mitindo iliyokuwa ikichezwa na kupendwa kwa wakati huo ya kizungu ni pop, ambayo mfalme wake alikuwa ni Michael Jackson. Sina haja sana ya kuelezea staili hii kwani wengi wanajua uchezaji wa Michael, ambapo kuna wakati ni kama vile bisi linavyotatarika linavyokaangwa kwenye sufuria.

Staili nyingine ni 'break dance.' Hii ni staili ngumu ambayo mchezaji ni lazima awe na ufiti wa viungo, vinavyoweza kunyumbulika na kuweza kupijipinduapindua kama mcheza sarakasi. Hii watoto wa mjini waliita 'mabreka'.

Halafu kuna 'funk' ambayo vijana wakati ule waliita 'mafanki'. ni staili ambayo viungo kama mikono, mabega na vitu vingine tu hufanya kazi yake. Kulikuwa na 'heavy funk' na 'slow funk'

Kwa upande wa staili za muziki wa Congo, miaka ya 1990, ndipo kulipokuwa na mitindo ya 'Kwasakwasa', 'Tshamukwale', 'Nzawisa', na 'Ndombolo ya Solo.'

Athari za mitindo hii ni bendi za Empire Bakuba chini ya uongozi wake marehemu Kabasele Yampanya 'Pepe Kalle', Bozi Boziana, Koffi Olomide, Wenge Musica, Kanda Bongo Man, Aurus Mabele na Loketo Group na hata Nouvelle Generation Zipompapompa chini ya uongozi wa Luciana Domingongo.

Ikumbukwe kuwa miaka hiyo wanamuziki kama Pepe Kalle na kundi lake walikuwa wakizuru sana nchini Tanzania na ndiyo miaka ambayo walitunga nyimbo kama 'Yanga Afrika' wakisifia timu ya Yanga na walipokuja baadaye na kuondoka wakatunga wimbo wa 'Hidaya', lakini pia upo wimbo mwingine ambao haukupata maarufu sana lakini ulikuwa ni baada ya ziara yao hapa nchini ukitungwa na kuimbwa na Papy Tex kwa lugha ya kiswahili, 'Mpenzi Bupe'.

Ikumbukwe kuwa miaka hiyo hiyo ya 1990, ndipo mwanamuziki Kanda Bongoman alipozuru nchini na kufanya onyesho kwenye Hoteli ya Kilimanjaro jijini Dar es Salaama, kiingilio ikiwa ni Sh.100,000 za Kitanzania. Kumbuka hicho kiingilio cha miaka hiyo ya 1990, lakini umati ulijaa kiasi kwamba kuna watu walizuiwa kuingia wakiwa na pesa zao mkononi.

Sidhani kama kuna mwanamuziki wa Tanzania kwa sasa anayeweza kuweka kiingilio hicho akajaza watu kiasi kile.

Kuingia kwa televisheni, video, na ziara za wanamuziki hao, zilisababisha athari chanya na kuanza kuwapata wachezaji disco ambao waliondokea kuwa maarufu sana.

Black Moses ni mmoja wa wacheza disco wa viwango vya juu aliyepata kutokea nchini Tanzania.

Huyu jamaa ambaye jina lake halisi ni Mussa Simba, kutwaa ubingwa wa Taifa kwake haikuwa jambo kubwa sana kwake. Alikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza miziki, wenyewe wanaiita wa kizungu, 'funk', 'pop' na 'break dance'.

Black Moses ambaye ni marehemu, kulikuwa kunawaka moto kama mpinzani wake akiwa Bosco Cool J ambaye alikuwa akimpa tabu na upinzani mkali sana.

Ilikuwa ni hatari sana kwenye kumbi za Vijana Social Hall, Kwa Macheni, Lang'ata Social Club, Bahama Mama.



Siyo picha za Michael Jackson, ni John Maganga mchezaji disco maarufu nchini maarufu sana miaka ya 1990 hadi mwishoni mwa miaka hiyo, ambapo si tu alicheza mithili ya mwenyewe, lakini hata wajihi wake alivyojitengeneza, uliwashangaza wengi kwa mfanano.



Mchezaji disco maarufu miaka ya 1990 Mussa Simba, maarufu kama Black Moses akiwa kwenye moja ya mashindano ya kusaka bingwa wa Taifa.

Kuna kijana mmoja kutokea Mwanza aliitwa John Maganga. Ni mcheza disco aliyejitengeneza na kufanana kabisa na Michael Jackson kiasi cha kushangaza wengi. Aliitwa Michael Jackson wa Tanzania. Wajihi wake, nguo, na hata alivyojitengeneza mwenyewe ilikuwa kama unakutana naye, unaweza kusema Michael.

Yeye kwa kiasi kikubwa alizitendea sana haki nyimbo za Michael kwenye uchezaji na kusababisha asiwe na mpinzani kwenye eneo hilo.

Unamkumbuka Prince Max? Yule aliyekuwa muigizaji ambaye wajihi wake kwa sasa unafanana sana na mwigizaji wa sasa Mkwere?

Pamoja na uigizaji, yeye pia alikuwa mahiri kwenye kusakata disco na mara nyingi anga zake zilikuwa kwa Macheni.

Ikumbukwe hata marehemu Banza Stone naye alianzia kwenye kusakata disco kabla ya nyota yake kuwaka zaidi kwenye muziki wa dansi.

Disco lilipambwa sana na wasanii kama Athumani Digadiga, Dogodogo Kadoda, Super Ngedere, King Jobiso, Small Jobiso na wengineo.

Kuna jamaa mmoja anaitwa Cadet Bongoman. Huyu alijipambanua na kujitengeneza kama Kanda Bongoman mwenyewe akivaa mapama na nguo kama mwenyewe, huku akiwa ni mtaalam wa kucheza nyimbo zake tu.

Kama vile haitoshi kulikuwa na mtu mmoja aliyeitwa Kokoliko. Alikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza nyimbo za Kikongo wakati huo Zaire na hasa za Empire Bakuba ya Pepe Kalle.

Kwa wajihi, alifanana sana na rapa, pia dansa wa bendi hiyo Bileku Mpasi, jina lake halisi likiwa ni Djuna Mumbafu.

Kokoliko alikuwa akipenda kuvaa nguo kama Bileku, na hata bendi ya Empire Bakuba ilipokuwa ikifanya maonyesho yake nchini ilikuwa ikisafiri naye mikoani na kucheza pamoja na Bileku, kiasi cha kuonekana kama Kurwa na Dotto.

Msanii huyo alikuwa akimpelekesha vilivyo Bileku kiasi cha mwenyewe kumkubali mpaka kumuachia zawadi mbalimbali anapoondoka.

Wasanii hao na muziki wao wa disco walidumu kwa muongo mmoja, hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000 walipoanza kuzimwa na mambo mawili.

Moja utandawazi, ambapo watu wengi sasa walianza kumudu kumiliki televisheni majumbani, hivyo kuwa na uwezo wa kutazama wakiwa majumbani na taratibu maonyesho na kusababisha watu kupungua.

Tuma meseji 0716 350534

# Kampuni ya OceanGate inayomiliki Titan yatangaza kusitisha safari za baharini

**WASHINGTON,** MAREKANI

KAMPUNI ya OceanGate, ambayo inamiliki nyambizi ya Titan iliyozama mwezi uliopita na kuwaua abiria wote watano waliokuwa ndani yake, imesitisha shughuli za kampuni hiyo.

Kampuni hiyo ilichapisha barua ya mstari mmoja kwenye tovuti yake ikisema kuwa imesimamisha shughuli zote za uchunguzi na kibiashara.

Katika tovuti ya kampuni hiyo pia ilikuwa imetangaza ziara za visiwa vya Ureno vya Azores na Bahamas.

Uchunguzi unaendelea kuhusu jinsi chombo hicho kidogo cha majini kilipasuka katika ajali ya Titanic tarehe 18 Juni.

Katika uchunguzi huo unaoongozwa na walinzi wa Pwani ya Marekani, unalenga kuzuia ajali kama hizo kutokea katika siku zijazo.

Mpelelezi mkuu Kapteni Jason Neubauer, alisema mwezi uliopita kwamba walinzi wa Pwani wameagiza kufanyika kwa kiwango cha juu zaidi cha uchunguzi, na utaendeshwa kwa pamoja kwa ushirikiano na mamlaka za Canada, Uingereza na Ufaransa.

Uchunguzi utaweza kupendekeza kufunguliwa kwa mashtaka ya kiraia au ya jinai.

Tarehe 28, Juni walinzi wa Pwani walisema mabaki ya binadamu kutoka Titan yalipatikana na kurejeshwa nchi kavu na kuhitimisha hatua ya awali ya uchunguzi. Mamlaka hiyo ilisema mabaki hayo yatapelekwa kwenye bandari ya Marekani kwa uchunguzi zaidi.

Kapteni Neubauer alisema katika taarifa wiki iliyopita kwamba bado kuna kazi kubwa iliyobaki kwa wachunguzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa OceanGate, Stockton Rush (61), alifariki akiwa ndani ya Titan pamoja na abiria wengine wanne akiwamo mfanyabiashara wa Uingereza na Pakistani Shahzada Dawood (48), na mtoto wake Suleman (19), mfanyabiashara wa Uingereza Hamish Harding (58), na Paul-Henry Nargeolet (77), ambaye ni mpiga mbizi wa zamani wa jeshi la wanamaji la Ufaransa. **BBC**

# Maandamano yarindima kila kona nchini Kenya

**NAIROBI,** KENYA

POLISI nchini Kenya wamekabiliana na waandamanaji kwa kuwarushia mabomu ya machozi wakati wakielekea katikati ya jiji la Nairobi.

Maandamano hayo yaliyoitishwa na kiongozi wa Azimio, Raila Odinga, kupinga hali ngumu ya maisha unaosababishwa na serikali ya Rais Willium Ruto.

Tukio hilo lilijiri baada ya mkutano mkubwa uliofanyika katika uwanja wa kihistoria wa Kamukunji, uliohutubiwa na Odinga ambaye aliwataka wafuasi wake kuandamana.

Wakati mabomu hayo yakirushwa, baadhi ya wafuasi hao walisikika wakiomba maji ili kupunguza athari za gesi ya kutoa machozi.

Wengine walibeba maji kwenye chupa na kutumia vipande vya nguo kujikinga dhidi ya vitoa machozi.

Hata hivyo, maandamano hayo yaliendelea kusonga mbele licha ya polisi kurusha mabomu ya machozi mfululizo.

Wafuasi hao walikuwa wakiandamana kuelekea Central Park, karibu na eneo la Uhuru Park.

Akiongea kwenye mkutano wa Kamukunji, Raila alisema ni lazima wafike huko hata polisi wakijaribu kuwazuia.

“Kuna njia nyingi za kufika Roma wakifunga barabara moja tunatumia nyingine, leo hii Rome yetu inaitwa Central Park ndiyo tutakutana baada ya mkutano wa Kamukunji,” alisema.

Aliwataka wafuasi wake kuepuka ghasia na kuongoza maandamano ya amani hadi Central Park.

Vilevile alizindua ukusanyaji wa saini ili kuishinikiza serikali ya Rais William Ruto kuondoka madarakani.

Mkutano uliamsha maandamano nchini kote kuishinikiza serikali ya Rais William Ruto kubatilisha baadhi ya vipengele vya Sheria ya Fedha ya 2023.

Kabla ya kufanyika kwa mkutano huo, polisi wengi walionekana wakizunguka katika mitaa mbalimbali ya mji huo mkuu na mingine kwenye mikoa mbalimbali ya nchi hiyo.

Maandamano yameripotiwa kufanyika katika maeneo kadhaa ikiwamo Mombasa na Kisumu na huko polisi wametumia mabomu ya machozi kuwatawanya watu.

Vyombo vya habari nchini humo vinasema kuwa biashara kadhaa zimeharibiwa na waandamanaji mjini Kisumu.

Makabiliano kati ya polisi na waandamanaji yameripotiwa katika maeneo kadhaa ya Nairobi na barabara kuu yenye shughuli nyingi kuelekea mjini ilikuwa imefungwa asubuhi.

Mamlaka iliruhusu mkutano huo kufanyika lakini ilionya dhidi ya waandamanaji wanaoingia katikati mwa jiji la Nairobi.

Maandamano hayo yanakuja baada ya Rais William Ruto kutia saini nyongeza ya ushuru yenye utata ikiwa ni pamoja na ile ya kuondoa ruzuku ya mafuta. **BBC**



Mchunga mifugo akitembeza kondoo wake barabarani katika wilaya ya Fayzabad mkoa wa Badakhshan nchini Afghanistan juzi. **PICHA: AFP**

# Wagner waondoka Afrika ya Kati

**NANGI,** AFRIKA YA KATI

WANAJESHI 600 kutoka kundi la mamluki la Wagner, wameondoka Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), ambako walikuwa wakifanya kazi na serikali.

Kulingana na gazeti la Le Democrate linalomilikiwa na watu binafsi liliripoti, kuwa wanajeshi hao wanaondoka nchini humo kutokana na hali kubadilika baada ya uasi uliofanywa na kundi hilo nchini Russia.

“Katika siku za hivi karibuni, imebainika kuwa vipengele vya kikundi cha Wagner viko katika mwelekeo tofauti. Kwa maneno mengine, wanaondoka Jamhuri ya Afrika ya Kati,” gazeti hilo lilisema.

Iliongeza kuwa kuondoka huko kunafuatia jaribio la uasi lililoanzishwa na kiongozi wao Yevgeny Prigozhin mwezi Juni dhidi ya serikali ya Vladmir Putin.

Kundi la utetezi la All Eyes on Wagner jana lilisema kuwa kati ya mamluki 500 na 600 wa Wagner wameondoka katika nchi hiyo.

Hatua hiyo inakuja wakati Russia ikiahidi kuwabakisha wakufunzi wa kijeshi nchini CAR na Mali licha ya uasi wa Wagner.

Kujiondoa huko kuliripotiwa karibu wiki moja baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergey Lavrov, kusema nchi za Afrika ziko huru kubaki na mamluki wa Wagner au kuwaruhusu waondoke.

Uasi wa Wagner mwezi uliopita ulisababisha maswali na wasiwasi juu ya mustakabali wa mamluki ambao wanafanya kazi nchini Mali, CAR na wanaaminika kuwa na uwepo nchini Burkina Faso na Sudan.
**BBC**

# MAONYESHO YA 47 YA BIASHARA YA KIMATAIFA YA DAR ES SALAAM



Mkurugenzi Mkuu wa Tigo, Kamal Okba (katikati), akipata maelezo alipotembelea banda la Tigo katika maonyesho ya 47 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam viwanja vya Mwalimu Nyerere, barabara ya Kilwa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Sehemu ya umati wa wananchi wakifika kwenye kilele cha maonyesho hayo jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wasukuma mkokoteni wakiwa wamepakia viti vikipelekwa kwenye mabanda ya maonyesho hayo, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mkonge Tanzania, Saddy Kambona (katikati), akitoa maelezo kwa raia wa kigeni aliyetembelea banda la mkonge katika maonyesho hayo, jana. Kulia ni Ofisa Uhusiano na Mawasiliano wa bodi hiyo, Esther Mbusi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mtafiti Msaidizi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Beatrice Togo (kushoto), akielezea kuhusu jiwe madini, lililo na viinilishe, ambalo limebuniwa na kutengenezwa na taasisi hiyo, linalosaidia wanyama wa kufugwa hususan msimu wa kiangazi, ambao huwa na malisho machache, wakati wa maonyesho hayo, jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**




Meneja mauzo wa kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Poul Msuku, akielezea ubora wa magari ya FAW zilizounganishwa katika kiwanda cha hapa nchini cha GFA kwa wateja waliotembelea banda lao katika maonyesho hayo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-16

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Kwa hili pekee, Eddy alijua kabisa kuna jambo ambalo si la kawaida. Kama alikuja Dar kwa nia nzuri kwa nini adanganye? Kwanza kwa nini asirudi na wenzake Dodoma halafu akapanda ndege kuja Dar? Kwa nini aliwadanganya wafanyakazi wenzake kuwa anabaki Mwanza? Ni ukweli usiopingika kuwa aliyekuja Dar ndiye yeye na aliyelala Mwanza ni mtu mwingine aliyeamua kuandikisha jina lake. Kwa nini aandikishe jina lake? Eddy aligundua kuwa kulikuwa na nia ovu.

"Huyu si mtu mzuri, inabidi afuatiliwe. Amemtengeneza mtu Mwanza na kumpeleka kwenye hoteli ya Kangaroo, akatumia jina lake ili ionekane yeye alibaki huko, ili hata upelelezi ukifanyika ionekana siku ya mauaji alikuwa Mwanza. Halafu yeye akapanda ndege kuja Dar. Kufanya nini? Na siku aliyokuja ndiyo mjomba wa Tessy anasema mpwa wake hakuonekana." Akajiambia Eddy.

Kwa asilimia nyingi tu, Eddy alianza kuwa na wasiwasi kuwa huyu ndiye muuaji wa Tessy. Atampata vipi? Ushahidi ataupata na kukusanya vipi ili dunia iamini?

Alichofikiria tangu mwanzo ni hicho hicho kuwa siyo kumpeleleza yeye, ni kuanza kupeleleza nyendo zake siku hiyo alipotua Dar kutoka Mwanza. Aliishia kuondoka na taxi ambayo tayari Eddy alikuwa ameshainakili namba yake.

"Nitaanza kwa dereva taxi huyu, hapa nitaanza sasa kufuata nyayo moja baada ya nyingine za muuaji wa Tessy, ili kujua kama alimuua kwa mkono wake, alitumia watu, kwa nini alimuua kinyama kiasi hicho, na sababu ni nini? Wakati huo wote atakuwa akikusanya ushahidi ili ukipelekwa mahakamani asichomoke. Kazi ya mwisho ni kumtia mbaroni."

************************************

Ilikuwa ni kama 'sapraizi' hivi. Eddy alifika kwenye Uwanja wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, terminal 2. hatukutia gari yake. Alipata taxi za siku hizi za kukodisha kwa mtandao hadi maeneo ya Tazara, Dar es Salaam. Baada ya hapo akagombea daladala linalokwenda Gongolamboto, akashukia kituo kilichopo karibu na uwanja huo.




Hakuna kitu alichofanya kwa bahati mbaya. Kila kitu alikifanya kwa makusudi. Alitaka kuonekana kama raia mwingine wa kawaida aliyeshuka kwenye daladala, ili kuondokana na kuwavutia watu au mtu yoyote ambaye angetaka kumpeleleza.

Baadhi ya wapelelezi huvutiwa zaidi na watu ambao wanaonekana wanajiweza kidogo, wanaoshuka na taxi, au wanaokuja na magari yao.

Akiwa amepachika kibegi chake cha uongo na kweli kwenye bega, alifuatana na baadhi ya watu waliokuwa wanakwenda uwanjani hapo kwa sababu mbalimbali.

Alipofika alikwenda kukaa kwenye benchi moja. Akachukua simu yake ya mkononi, akampigia Maria.

"We mwanamama nipo hapa kwenu hebu njoo."

"He upo wapi?"

"Nipo nje ya ofisi yenu hapa, ukitoka utaniona, nimekaa kwenye benchi."

"He mwenzetu umekuwa na yale yale au mengine?"

"Yapi?" Akauliza Eddy Kamal.

Umenifuata mimi unipe lanchi kama ulivyosema siku ile, au yale mambo ya yule jamaa?" Ilisikika sauti ya Maria masikioni mwa Eddy.

"Yote mawili. Nataka kuua ndege wawili kwa jiwe moja."

"Haya, nipe dakika tano nije kukuona." Dakika sita baadaye macho ya Eddy alifanikiwa kumuona mwanadada mmoja akiangazaangaza.

**"Wewe si ulinipa video ya yule jamaa, bado wewe sasa." Akazungumza kwa mzaha.**

"Nipo huku." Akamshtua.

"He Eddy jamani, ngoja nikuwao!" Bila kujizuia Maria akamkubatia Eddy ambaye mara mwisho kumuona ilikuwa ni miaka miwili nyuma kwenye sherehe za harusi.

Ilikuwa ni harusi ya Maria mwenyewe. Kabla ya kuolewa alikuwa kwenye mikono ya Eddy. Maana yake waliokutana hapo ni wapenzi wa zamani. Ni wiki kadhaa tu mawasiliano yao walianza tena kwa njia ya simu ya email, na yote ni kwa sababu ya sakata hili linaloendelea.

"Hivi, huogopi video itakayopelekwa kwa mumeo?" Eddy alimstua kwa swali hilo baada ya kumaliza kukumbatiana na kusalimiana kwa bashasha.

"Utapeleka wewe hiyo video?" Maria akamuuliza.

"Siku hizi bwana usiamini chochote, usijiamini hata kama uko peke yako chumbani, kunaweza kukawa na kamera inakuchukua tu, ukajichekeshachekesha, halafu kesho watu wakaipata wakakuona kama mwehu."

"Bwana ee, mimi ndiyo nikakukumbatia, nisimkumbatia mgeni wangu, kisa naogopa kamera..."

"Wewe si ulinipa video ya yule jamaa, bado wewe sasa." Akazungumza kwa mzaha.

"Na wewe nawe hujaacha tu mizaha yako. Enhee haya tunakwenda wapi lanchi, mimi ndiyo nishaaga ofisini."

"Maria, mimi nimekuja hapa mara moja tu, wala sina muda wa kupoteza."

"Umeenza hivyo we mwanaume, yaani umekuja huku halafu hutaki kunipeleka lanchi, huyu uliyempata usimuche."

"Sijampata yoyote tangu niachane na wewe, wote niliokutana nao matapeli tu, najuta kumuachia jamaa mzigo, ningekuona mwenyewe tu." Akasema Eddy na alipomaliza akakutana na kicheko kikali kutoka kwa Maria.

"Ulisema cha nini, wenzio wakasema nitakipata lini." Akazidisha utambi.

"Dunia duara, kama ni riziki yangu nitaipata tu."

"Wapi baba tayari nina mtoto mwenzio."

"Hata ungekuwa nao kumi, kama nitakuhitaji basi ni wewe, watoto mimi hawanipi tabu." Aliingiza mfukoni na kutoa noti tatu za Sh. 10,000 akamkabidhi Maria.

"Hiyo ndiyo lanchi yako kwa leo. Nilitamani sana twende tukale wote ili unilishe, sijalishwa siku nyingi sana."

Maria akaendelea kuvunjika mbavu.

"Nitapata tu muda, nitarudi tena hapa, siyo kikazi, ila kwa ajili yako tu, utafurahi." Eddy akamalizia na kumnong'oneza kitu masikioni ili kisisikike kwa mtu yoyote.

"Haya baba fanya kazi yako." Akajibu Maria huku akishukuru na akamkumbatia na kumbusu tena.

Maria aliondoka taratibu akirudi ofisini huku akigeuka mara kwa mara kumtazama Eddy.

Alipohakikisha Maria ameondoka alitoka taratibu kwenda sehemu ambayo tax huwa zinapaki.

Alikwenda hapo kwa nia moja tu, kuisaka ile taxi aliyoiona kwenye video aliyotumiwa na Maria. Namba alikuwa ameshaziandika kwenye mkono wake wa kushoto. Kwa mbinu za hali ya juu hakuonekana kama analitafuta.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AFANDE SELE AACHIA WIMBO WA MAZINGIRA, WENYE SAUTI YA RAIS SAMIA, DK MPANGO

**Mwandishi Wetu, Morogoro**

MWANAMUZIKI Mkongwe wa muziki wa kizazi kipya , Selemani Msindi 'Afande Sele', ameachia wimbo wake mpya wa mazingira, wenye sauti ya Rais Samia Suluhu Hassan na makamu wa Rais, Dk Philip Mpango.

Mwanamuziki huyo ambaye pia ni Balozi maalumu wa mazingira nchini ameachia ngoma hiyo juzi pamoja na kutambulisha rasmi Taasisi yake (ASEFO) itakayofanya kazi za mazingira na maji nchini ikishirikiana kwa karibu na Serikali na wadau wengine.

Moja ya majukumu ya ASEFO ni kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu utunzaji wa mazingira kote nchini, faida za kuyatunza na athari zake pale yanapoharibiwa, umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji na kuwa na mashamba darasa.

Akizungumza juzi, makao makuu ya ASEFO, Chamwino Manispaa ya Morogoro, Afande Sele alisema mbali na kuelimisha kupitia nyimbo mbalimbali anazoendelea kutunga, ukiwemo wimbo wa ' Rais Samia Kasema' alioutambulisha juzi ambao tayari umeanza kusikika kwenye 'platforms' mbalimbali, pia Taasisi hiyo itakuwa na kazi maalumu ya kufundisha na kuhamasisha kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira.

Wimbo huo ambao huko kwenye audio una sauti ya Rais Samia na makamu wa Rais, Dk Mpango wakimsisitiza Afande Sele kutunga nyimbo zenye ujumbe wa kutunza mazingira ambazo zitatoa elimu kwa jamii kipindi hiki ambacho dunia inapambana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi.

"Mbali na kutunga nyimbo za Mazingira, ASEFO pia itakuwa na programu ya kupanda miti katika maeneo mbalimbali, kutoa elimu ya uhifadhi mazingira na vyanzo vya maji, tutakuwa na mashamba darasa na mambo mengine mengi ya uhifadhi wa mazingira na kulinda vyanzo vya maji tukishirikiana na Serikali, Taasisi, kampuni na mashirika mbalimbali," alisema Afande Sele na kuongeza,

"Lengo letu ni kuleta mageuzi katika utunzaji wa mazingira, tutajikita kwenye mambo mbalimbali ya mazingira, ikiwamo kupanda miti ambayo tutahakikisha inatunzwa na kulelewa kama ambayo analelewa mtoto ili makuzi yake yawe bora na isaidie kuboresha mazingira yetu, kwani mazingira ni uhai," alisema Afande Sele.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa taasisi ya 'Unganisha Environment Conservation Organization (UECO)', Sophia Kalinga alisema ujio wa ASEFO utasaidia kuongeza nguvu kupambana kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira nchini.

"Athari za uharibifu wa mazingira ni tatizo kubwa kwa jamii ambayo haina elimu ya kutosha ya utunzaji wa mazingira licha ya juhudi za kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira inatoa mwanga baada ya serikali, taasisi binafsi na mashirika kusimama kidete kutoa elimu ya kuyatunza mazingira nchini."alisema Sophia.

Aidha, Mgeni rasmi katika uzinduzi wa taasisi hiyo ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chuo ch Mtakatifu Joseph, Seif Chomoka alisema kuzinduliwa kwa ofisi ya Taasisi ya Afande Sele ni hatua nzuri ambayo itakuja kuleta mabadiliko ndani ya Manispaa ya Morogoro na Tanzania kiujumla.

"Moja ya mambo mnayopaswa kuyafanya uongozi wa ASEFO ni kuwa Taasisi ya mfano kwa kuanza kupanda miti na kuitunza ili kupata msitu utaokuwa wa mfano kwa mashirika, taasisi binafsi na serikali za utunzaji wa mazingira kuiga kama njia ya kukabiliana na maeneo yaliyoharibiwa."alisema Chomoka.

Chomoka alisema jamii inahitaji zaidi kujifunza kwa vitendo na pale watapoona mfano halisi ni rahisi kuiga na kuleta manufaa ya pamoja kwa wao kupanda miti na kuitunza.



Mkurugenzi Mtendaji wa Chuo cha St Joseph, Seif Chomoka (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua Ofisi ya Taasisi ya Afande Sele (ASEFO) iliyopo Chamwino, Manispaa ya Morogoro, kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Seleman Msindi (Afande Sele). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi ZFF kujulikana leo Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MKUTANO Mkuu wa Uchaguzi Mkuu wa shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF) unafanyika leo Visiwani Zanzibar kwa ajili yakuwapata viongozi wapya wa chombo hicho cha kusimamia soka.

Uchaguzi huo unafanyika ukiwa ni wa pili baada ya Shirikisho hilo kufanya mabadiliko ya katiba yake kutoka kwenye Chama (ZFA)na kuwa katika muundo wa Shirikisho (ZFF).

Katika Uchaguzi huo jumla ya wagombea watatu wanawania nafasi ya Urais huku Rais anaemaliza muda wake Abdulatif Ali Yassin jina lake liliondolewa katika kinyang'anyilo hicho kwa kutokuwa na sifa kwa mujibu wa Kamati ya uchaguzi ya ZFF.

Wagombea hao ambao wanachuana vikali ni Suleiman Mahmoud Jabir, Kamal Abdulsatar na Juma Hassan ambapo kila mgombea alipata fursa ya kutaja vipaumbele vyake katika kipindi cha kampeni.

Akizungumza na Nipashe katibu wa Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, Habibu Mshindo Abdallah alisema maandalizi yote ya kuelekea uchaguzi huo yamekamilika.

Alisema, katika kipindi chote cha mchakato wa uchaguzi wagombea wote walifata kanuni ya uchaguzi Kwa kufanya kampeni kwa mujibu wa kanuni.

"Mpaka kufikia leo hii (jana) hakuna jambo lolote la kinyume na katiba au kanuni ya uchaguzi lililojitokeza likasababisha mgombea kutoendelea na mchakato wa uchaguzi, kila kitu kipo sawa na tunasubiri kesho (leo) wajumbe wapige kura," alisema Abdallah.

Aidha, alisema katika uchaguzi huo wapiga kura ni Makatibu wa Vilabu 16 vya Ligi Kuu ya Zanzibar, wenyeviti na makatibu wa vyama vya mikoa, Chama cha Haki na hadhi za wachezaji, Chama cha Makocha, Chama madaktari michezoni na Chama cha Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu.

Kwa mujibu wa katiba ya (ZFF) Uchaguzi Mkuu unafanyika kila baada ya miaka minne kuanzia ngazi zote wilaya Mkoa na Taifa.

## Karate Taifa kushiriki mashindano Maziwa Makuu

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya mchezo wa Karate ikiwa na wachezaji 20 inatarajiwa kuondoka nchini Julai 15 kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kushiriki mashindano ya mchezo huo kwa nchi za Maziwa Makuu yatakayofanyika nchini humo kuanzia Julai 17-23 mwaka huu.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, kiongozi wa Chama cha Karate Tanzania, Herman Kiwili alisema maandalizi kuelekea kwenye michuano hiyo yanaendelea vyema.

"Timu inaendelea vizuri na mazoezi lengo letu ni kwenda kufanya vizuri na kuweza kuipeperusha vyema bendera ya Taifa letu," alisema Kiwili.

Alisema zaidi ya nchi 10 zinatarajiwa kushiriki mashindano hayo na kudai timu ya Tanzania itaondoka hapa nchini siku hiyo ya Julai 15 ikiwa na msafara wazaidi ya watu 20 wakiwemo wachezaji, viongozi na makocha.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi zote za maziwa makuu na tayari zimeshathibitisha ushiriki wake.

Nchi hizo za Maziwa Makuu zinazotarajiwa kushiriki mashindano hayo zinajumuisha, Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Ethiopia, Malawi, Msumbiji, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Angola

## BMT yavitaka vyama kujisajili kwa wakati

**Na Shufaa Lyimo**

BARAZA la Taifa la Michezo( BMT) limevitaka vyama vya michezo vya Taifa kufanya usajili wake kwa wakati ili wapate urahisi wa kufanya kazi zao bila vizuizi vyovyote.

Wito huo ulitolewa jana na Baraza hilo kupitia kwa Ofisa habari wake Najaha Bakari wakati wa kilele cha maadhimisho ya maonyesho ya Kimataifa ya biashara ya sabasaba yaliyoambatana na siku ya kiswahili Duniani.

"Tunaomba wadau mbali mbali wa michezo wafanye usajili wa vyama vyao ili wapate muda wa kuviendesha vyama hivyo, kuendesha chama cha michezo bila kupata usajili ni kosa kisheria, sasa ili kuepuka usumbufu ni vizuri kuvisajili BMT mapema ili kuepuka mikwamo yoyote," alisema Najaha.

Alisema chama chenye usajili kinakuwa kinatambulika rasmi na kitakuwa kikifanya kazi zake kwa uhuru na kupata kuungwa mkono na Serikali.

Katika hatua nyingine jana BMT imeadhimisha siku ya kiswahili Duniani kwa kuchezwa michezo mbalimbali ikiwemo bao, Karate, Netiboli, Kikapu pamoja na burudani mbali mbali kutoka kwa wasanii wa Muziki na vichekesho akiwemo Mrisho Mpoto 'Mjomba' na na Joti.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ONANA AKARIBIA MAN

KLABU ya Manchester United inakaribia kumsajili kipa wa Inter Milan, Andre Onana mwenye umri wa miaka 27 baada ya kuafikiana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Cameroon. **(Fabrizio Romano)**

### HOJLUND PIA ATAKIWA

MASHETANI Wekundu hao pia wanapanga kumnunua mshambuliaji wa Atalanta na Denmark, Rasmus Hojlund mwenye umri wa miaka 20 kwa pauni milioni 50. **(Telegraph)**

### CAICEDO MIL 100

CHELSEA italazimika kulipa zaidi ya pauni milioni 100 ikiwa inataka kumsajili kiungo wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21 msimu huu wa joto. **(Telegraph)**

### BONUCCI ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inajiandaa kumnunua beki mkongwe wa Italia na Juventus, Leonardo Bonucci mwenye umri wa miaka 36, ili kuongeza uzoefu katika msimu ujao wa a Ligi ya Mabingwa Ulaya. **(TEAMtalk)**

### TIMBER NA ARSENAL

JURRIEN Timber wa Ajax jana Ijumaa alifanyiwa vipimo vya afya pale Arsenal ili kukamilisha dili la pauni milioni 38.5 kwa beki huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 22. **(Standard)**

### PERISIC KUONDOKA

KIUNGO wa Tottenham Hotspur, Ivan Perisic amemwambia kocha, Ange Postecoglou kwamba, ana nia ya kusitisha mkataba wake, huku raia huyo wa Croatia mwenye umri wa miaka 34 akitaka kujiunga na Hajduk Split. **(Gianluca Di Marzio)**

### HOJBJERG AWANIWA

KLABU ya Atletico Madrid imewasiliana na kiungo wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 27, ambaye pia amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda Bayern Munich. **(Mail)**

### LAVIA ANYATIWA

KLABU ya Southampton inaamini kuwa itapewa bei inayotakiwa ya pauni milioni 50 inapojiandaa kumnunua kiungo wa kati wa Ubelgiji, Romeo Lavia mwenye umri wa miaka 19, huku Chelsea, Liverpool na Arsenal pia zikiwania saini yake**. (Sky Sports)**

### ZAHA AGOMBEWA

MATUMAINI ya Crystal Palace kumnunua tena Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 30 yamefifia huku mshambuliaji huyo akizingatia ofa kutoka Lazio, Fenerbahce na Al-Nassr. **(Standard)**

### WILLIAN MKATABA MPYA

FULHAM inakaribia kumpa mkataba mpya Willian baada ya mshambulizi huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 34, kuwa mchezaji huru mwishoni mwa juma lililopita. **(The Athletic)**

### SALIBA AONGEZEWA

MLINZI wa Arsenal, William Saliba mwenye umri wa miaka 22 ametia saini mkataba mpya utakaomweka pale uwanja wa Emirates hadi mwaka 2027. **(The Athletic)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# JESUS: GUARDIOLA ALINITOA MACHOZI MANCHESTER CITY

●●●Mbrazil huyo alidumu kwenye kikosi hicho cha Etihad kwa miaka mitano kabla ya kuamua kujiunga na Arsenal...

**LONDON, England**

GABRIEL Jesus amesema aliamua kuondoka Manchester City wakati kocha Pep Guardiola alipomtoa machozi baada ya kumuacha nje ya kikosi kilichoanza katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alicheza chini ya Guardiola kwa miaka mitano katika uwanja wa Etihad kabla ya kujiunga na Arsenal msimu uliopita wa joto, hatua ambayo alisema ilimfanya ajisikie "huru."

Akizungumza katika kipindi cha televisheni cha ESPN cha Denilson show, Jesus alisema mabadiliko katika maisha yake ya City yalikuja wakati wa mchezo wao wa nyumbani dhidi ya Paris Saint-Germain Novemba mwaka 2021 alipowekwa benchi.

"Kulikuwa na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya PSG nyumbani, ambapo alimweka Oleksandr Zinchenko kama 9. Jambo la kichaa," alisema Jesus.

"Siku moja kabla, hakumtumia Zinchenko kwenye mazoezi, aliniweka mimi kama mshambuliaji... na hata Zinchenko aliniambia: 'siku ile nilijisikia vibaya kwako.'

"Saa mbili kabla ya mchezo kuna mazungumzo ya timu, timu inakula, inapumzika kwa dakika 30 na kwenda mchezoni, akatuambia timu itakavyokuwa, hata sikula, niliienda moja kwa moja chumbani huku nikilia, nikampigia simu mama yangu na kumwambia: 'Nataka kuondoka.'

Jesus alichukua nafasi ya Zinchenko kipindi cha pili na kutengeneza bao la kusawazisha kabla ya kufunga bao la dakika za mwisho na kuipa City ushindi wa 2-1.

"Nilijisikia vibaya. Dakika tano baada ya Kylian Mbappe kufunga bao 1-0, Guardiola aliniita. Nilitoa pasi ya bao na kufunga; tuligeuza matokeo kuwa 2-1. Katika mchezo uliofuata Ligi ya Mabingwa wa ushindi wa 2-1 dhidi ya RB Leipzig, nilifikiri nitacheza, lakini sikucheza.

"Kulikuwa na mengi ya hayo kwa Guardiola. Ni ngumu sana. Hapo ndipo nilipoamua na sikutaka kubaki tena. Niliamua kuondoka. "

Jesus alijiunga na City Januari 2017 kutoka Palmeiras ya Brazil na kushinda mataji 11 akiwa na klabu hiyo.

Wakati wa msimu wake kwanza akiwa Arsenal, alifunga mabao 11 na kutengeneza mengine saba katika mechi 26 za ligi walipomaliza washindi wa pili nyuma ya City kwenye Ligi Kuu England.

# SILVA ATENGEWA MSHAHARA MNONO SAUDIA




**LONDON, England**

BERNARDO Silva anapewa ofa, mshahara wake kuongezwa mara tatu zaidi wa ule wa Manchester City akikubali kuhamia Klabu ya Al Hilal ya Ligi Kuu ya Saudi Arabia, kwa mujibu wa ESPN.

Silva anapokea kiasi cha pauni 150,000 kwa wiki pale kwenye uwanja wa Etihad, lakini anashawishika kuhamia Saudi Arabia kwa mshahara wa karibu pauni 500,000 kwa wiki.

Silva yuko tayari kutafuta changamoto mpya msimu huu wa joto baada ya miaka sita akiwa City.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba anapendelea kubaki Ulaya, lakini bado hajakataa kuungana na Ruben Neves na Kalidou Koulibaly katika Klabu ya Al Hilal.

Silva amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake na City na watadai ada kubwa kabla ya kumruhusu kuondoka, lakini hilo haliwezekani kuwa tatizo kwa timu hiyo ya Saudi Pro League.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Paris Saint-Germain na Barcelona pia wana nia lakini hawajathibitisha nia yao kwa ofa rasmi.

Vyanzo hivyo viliongeza kuwa City wako tayari kumpa Silva mkataba mpya, lakini hautalingana na mshahara unaopendekezwa na Al Hilal.

Klabu ya Saudia, kulingana na vyanzo, ilikutana tena na wawakilishi wa Silva wiki iliyopita.

Kocha Pep Guardiola anavutiwa sana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, lakini vyanzo vimeiambia ESPN kwamba klabu haitamzuia kama ataamua kuondoka na watapokea ofa nzuri.

Wakati huo huo, vyanzo viliiambia ESPN kwamba mshambuliaji wa zamani wa Manchester United, Jesse Lingard pia anawindwa na huko Saudia.

Lingard ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Nottingham Forest mwishoni mwa msimu uliopita, amerejea kutoka mapumzikoni kutoka Marekani na anafanya mazoezi pale Manchester kabla ya kuamua uhamisho wake mwingine.

Lingard mwenye umri wa miaka 30 alicheza mechi 20 akiwa Forest msimu uliopita, akifunga mara mbili.

# Xhaka atua Leverkusen

**MUNICH, Ujerumani**

GRANIT Xhaka amejiunga na Bayer Leverkusen akitokea Arsenal, na hivyo kumaliza miaka saba ya kiungo huyo kukaa Kaskazini mwa London.

Mchezaji huyo wa Uswisi mwenye umri wa miaka 30 alijiunga na Washikabunduki hao kutoka Borussia Monchengladbach mwaka 2016 na kufanikiwa kuichezea klabu hiyo mechi 297. Amesaini mkataba wa miaka mitano pale Leverkusen.



Mara baada ya kukamilisha usajili huo, Xhaka alisema: "Ninaijua ligi ndani na nje, nimekuwa nikiwatazama kutoka London.

"Leverkusen ni klabu yenye historia ya kuvutia na malengo makubwa. Zaidi ya yote, naiona kama klabu yenye mustakabali mzuri. Majadiliano na wale waliohusika yalikuwa ya kutia moyo sana."

Mkurugenzi wa michezo wa Leverkusen, Simon Rolfes nae alisema: "Kumpata Granit ni ushindi mzuri, kwa sasbabu ni mmoja wa wanasoka bora kabisa.

"Ubora wake wa soka unajulikana kila mahali. Lakini juu ya yote, kuna wachezaji wachache ambao kutokana na mawazo yake bora na haiba yake, wanaweza kuongoza timu kwa kushawishi awezavyo."

Xhaka alishinda mataji mawili ya FA na Ngao mbili za Jamii wakati wa maisha yake England.

Alifanywa kuwa nahodha na bosi wa wakati huo, Unai Emery Septemba 2019, lakini kitambaa hicho kiliondolewa chini ya miezi miwili baadaye baada ya utata wake.

Mikel Arteta alimtambulisha tena mhitimu huyo wa akademi ya FC Basel kwenye kikosi cha kwanza baada ya kuteuliwa baadaye mwaka huo, huku Xhaka akicheza mechi zote isipokuwa moja ya ligi kuu ya Arsenal msimu uliopita walipomenyana na Manchester City.

Sasa ataungana na kiungo wa zamani wa Liverpool na Real Madrid, Xabi Alonso, ambaye aliiongoza Leverkusen hadi nafasi ya saba kwenye Bundesliga muhula uliopita.

## Azpilicueta aondoka Chelsea baada ya miaka 11

**LONDON, England**

NAHODHA wa Chelsea, Cesar Azpilicueta ametangaza kuachana na klabu hiyo ya Ligi Kuu England baada ya kukaa pale Stamford Bridge kwa miaka 11.

Azpilicueta anaondoka Chelsea kwa makubaliano huku akiwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Atletico Madrid wanakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili beki huyo kwa uhamisho wa bure.

"Cesar ameacha alama ya milele Chelsea, kama shujaa, kama bingwa, na kama gwiji mwaminifu wa Chelsea," alisema Todd Boehly, mwenyekiti wa Chelsea, na Behdad Eghbali, mmiliki mwenza wakiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Ameweka viwango katika klabu kwa zaidi ya muongo mmoja na kuonesha kila mtu kile kinachohitajika siku hadi siku ili kupata mafanikio.

"Makocha na wachezaji wenzake wa zamani na wa sasa wamemwamini kuongoza kwa mfano kama nahodha. Amefanya hivyo kwa ukamilifu ndani na nje ya uwanja, jambo ambalo tunashukuru. Kwa hayo na mengine mengi, Cesar atakaribishwa kila mara kurejea Stamford."

Kocha mkuu wa Atletico, Diego Simeone alijaribu bila mafanikio kumsajili katika madirisha ya awali ya uhamisho.

Azpilicueta pia alilengwa na Barcelona msimu uliopita wa joto, lakini badala yake aliamua kuongeza mkataba wake Chelsea.

Katika misimu 11 akiwa Stamford Bridge, alicheza mechi 508, zikiwemo 32 msimu uliopita. Alishinda mataji mengi akiwa Chelsea ikiwa ni pamoja na mawili ya Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya.



# SINGIDA FG YAUTAKA UBINGWA LIGI KUU, YAAMUA KUWEKA KAMBI JIJINI ARUSHA

**Saada Akida na Abdallah Mataka**

WAKATI Uongozi wa klabu ya Singida Fountain Gate ukihairisha kwenda kuweka kambi yao nchini Tunisia, Mshauri wa benchi la ufundi la klabu hiyo Christopher Hughton amesema kama wachezaji na makocha watazitumia vizuri siku watakazoweka kambi kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu na Mashindano ya Kimataifa, wanayo nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi kuu Tanzania Bara.

Uongozi wa timu hiyo jana ulitangaza maamuzi ya kwenda kuweka kambi Karatu mkoani Arusha na kuachana na mipango ya awali ya kwenda kuweka kambi Uturuki kujiandaa na msimu mpya wa mashindano wa 2023/2024.

Akizungumza na gazeti la Nipashe, Hughton alisema kuwa maboresho ambayo wameyafanya ikiwemo usajili umekifanya kikosi hicho kuwa bora zaidi jambo ambalo linampa matumaini ya kutoa ushindani na kubeba mataji katika msimu mpya ambao unatarajia kuanza hivi karibuni.

"Tumesajili wachezaji wenye uwezo mkubwa lakini kingine kizuri ni kubakisha wachezaji wetu muhimu ndani ya timu, hivyo ni miongoni mwa vitu muhimu ambavyo vinaweza kutufanya kuwa bora zaidi," alisema Hughton.

akizungumza na gazeti hili kuhusu kambi ya timu hiyo, Ofisa habari wa timu hiyo, Hassan Masanza alisema uongozi wa timu hiyo kwa pamoja wameamua kwenda kuweka kambi mkoani Arusha.

Alisema awali maandalizi yalikuwa yafanyikie kwenye nchi ya Tunisia lakini kutokana na ufinyu wa muda na kuchelewa kukamilika kwa zoezi la usajili wa wachezaji wamelazimika kubaki nchini ili wachezaji wote waweze kushiriki maandalizi haya kwa wakati.

"Tuna sababu kubwa tatu za kutoenda Tunisia, kwanza ni muda, muda sio rafiki kwa kuwa tunatukio kubwa la siku yetu ya 'Singida Big Day', pia maandalizi ya mechi yetu ya ngao ya jamii na zoezi la usajili halijakamili, uongozi kwa kuyaona haya umeamua kambi yetu ifanyike hapa hapa nchini na tutaenda Arusha," alisema Masanza.

Alisema tayari kocha wa timu hiyo, Hans Van Pluijm ameandaa programu ya mazoezi itakayofanyika hapa nchini.



Mwenyekiti wa Maonyesho ya Sabasaba kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kanali Shija Lupi, (wa pili kulia), akicheza muziki na wafanyakazi wa banda la jeshi hilo jana, baada ya kupokea tuzo ya ushiriki bora wa maonyesho hayo jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha Azam aongeza dozi mazoezi

**Na Saada Akida**

KOCHA mpya wa Azam FC, Youssouph Dabo ameweka wazi ratiba ya mazoezi kwa wachezaji wake ambapo sasa watakuwa wakifanya mara mbili kwa siku ili kujiandaa vyema na msimu mpya wa ligi kuu na mashindano ya Kimataifa.

Azam FC JUmatano iliyopita walianza rasmi maandalizi ya msimu mpya wa 2023/24 wa Ligi Kuu Tanzania na michuano ya kimataifa kwa kufanya mazoezi mara moja asubuhi pekee lakini sasa wanaanza kufanya mara mbili kwa siku.

Akizungumza na Nipashe jana, Dabo alisema watakuwa na vipindi viwili vya mazoezi asubuhi na jioni kwa muda wote wa maandalizi yao ambapo amegawa kwa asubuhi kuangalia utimamu wa mwili kwa wachezaji wake na jioni kufanya mazoezi ya kiufundi pamoja na kuchezea mpira.

Alisema anachokifanya ni kuwajenga wachezaji wake kuwa na nguvu lakini pia kuwa wanyumbulikaji wanapokuwa na mpira .

"Katika mchezo wachezaji watafanya makosa kwangu sio tatizo, kubwa ni kuwa na tahadhari na kufanyia kazi kila kosa tunaloliona uwanjani, wachezaji wako vizuri na kulingana na usajili uliofanyika na maandalizi tutafanya vizuri msimu ujao, ni naamini hivyo" alisema Dabo.

Alisema mikakati yao ni kuona wanaanda timu itakayokuwa na ushindani na kutoa changamoto kwa timu nyingine kwenye ligi msimu ujao na kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kutwaa ubingwa.

Aidha, beki mpya wa timu hiyo, raia wa Senegal, Cheikh Tidiane Sidibe alisema anafurahi kuwa sehemu ya kikosi cha Azam FC atahakikisha atashirikiana vyema na wachezaji wenzake kufikia malengo yaliyowekwa na klabu. "Nina imani kubwa na kiwango changu, nitafanya vizuri na kuisaidia timu yangu kufikia malengo yanayotarajiwa kwa kushirikiana na wachezaji wenzangu, kikubwa ni kufuata yale maelekezo tutakayopewa na benchi la ufundi ili kufanya vizuri katika kila mchezo," alisema Sidibe.

Kikosi cha timu hiyo kinatarajiwa kuondoka nchini Jumapili kesho kuelekea nchini Tunisia katika mji wa Sousse aliozaliwa na kuishi aliyekuwa kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi kwa ajili ya kuweka kambi kujiandaa na msimu mpya wa mashindano.

# Nkane kutibiwa na Serikali

INATOKA UK. 24

"Nkame alipata shida, aligongana na mchezaji wa timu pinzani na baada ya hapo akaanguka vibaya ikasababisha kupoteza fahamu kwa muda, akapatiwa huduma ya kwanza haraka pale na naamini mliona kwenye televisheni kabla ya kukimbizwa hospitalini na akapata matibabu akarudi kwenye hali yake, lakini bado analalamika kusikia maumivu makali kichwani, mwenyewe amekuwa akisema kichwa kinamuuma, madaktari wa Malawi wakasema akifika Tanzania akafanyiwe vipimo na uchunguzi zaidi," alisema Kamwe.

Kutibiwa kwa Nkane kunaonyesha jinsi Serikali za nchi zote mbili zilivyowajibika kwa hali ya juu na ni mfano kwa taasisi zingine kuiga mfano huo mara linapojitokea suala kama hilo mchezaji anapokuwa chini ya mikono yao.

Mchezo huo wa juzi wa kimataifa wa kirafiki ulimalizika kwa timu hizo kutoka suluhu.

Katika hatua nyingine akizungumzia usajili, Kamwe alisema tayari wameshamaliza, usajili na kwa sasa wanasubiri kuwasili kwa Kocha wao, Miguel Angel Gamondi ili waweke majina ya nyota wao hadharani.

Aidha, alisema baada ya kukutana na kocha huyo watawatangaza wachezaji wao akiwamo mchezaji atakayevaa jezi namba sita ambayo kwa muda mrefu walikuwa wakiitangaza.

Alisema baada ya kutangaza wachezaji wao wataingia rasmi kambini kujiandaa na msimu mpya.

# Kouame, Ngoma wasaini miaka miwili Simba

INATOKA UK. 24

Kouame anakuwa mchezaji wa tatu wa kimataifa kutambulishwa na klabu hiyo akianza Mcameroon Willy Essomba Onana kutoka Rayon Sport ya Rwanda na Ngoma.

Mbali na wachezaji hao, Simba pia imewatambulisha watu wa benchi la ufundi ambao ni kocha wa magolikipa, Daniel Cadena raia wa Hispania aliyetokea Azam FC, kocha wa viungo, Corneille Hategekimana aliyetokea AS Kigali ya Rwanda na Meneja mpya wa timu na Mkuu wa Sayansi ya Michezo, Mikael Igendia.

Michezo
Jumamosi Julai 8, 2023
Nipashe



**Jesus: Guardiola alinitoa machozi Man City** UKURASA 21




Aubin Kramo Kouame. **PICHA: MTANDAO**

# NKANE KUTIBIWA NA SERIKALI

## ●●●Yanga yamshukuru Rais Samia kwa kuamua kugharamia matibabu ya nyota huyo aliyeumia Malawi...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuahidi kuwa serikali itagharamia na kusimamia uchunguzi wa afya ya mchezaji, Denis Mkane aliyeanguka na kuzirai kwenye mechi ya kuadhimisha miaka 59 ya uhuru wa Malawi dhidi ya Nyasa Big Bullets juzi.

Nkane aligongana na mchezaji wa Nyasa Big Bullets na kuzimia wakati mchezo huo ukiendelea juzi kwenye uwanja wa Bingu wa Mutharika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya kuwasili kutoka nchini humo, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe alisema klabu hiyo inamshukuru kwa dhati Rais Samia kwa kuhakikisha mchezaji wao anafanyiwa vipimo zaidi ili kubaini kama ameumia ili kupata matibabu anayostahili.

"Kipekee kabisa, tumpongeze na tumshukuru Rais wa Jamhuri wa Muungano, Dk. Samia Suluhu Hassan, alisema tukifika tu hapa nchini huyu kijana achukuliwe na madaktari wakamfanyie uchunguzi waone kama ameumia zaidi ya watu walivyoona pale Malawi, tunashukuru sana kwa kujali afya ya mchezaji wetu, alitoa agizo tukifika tu hapa nchini Nkane achukuliwe na kwenda kupatiwa matibabu, nadhani mmeona gari la wagonjwa na watu wa Serikali hapa uwanjani, Yanga tunashukuru sana," alisema Kamwe.

Akielezea jinsi alivyoumia, huduma ya kwanza na matibabu yaliyotolewa nchini Malawi, alisema yalikuwa ni mazuri na anawashukuru madaktari na wauguzi wote wa nchini humo kwa kumsaidia mchezaji huyo kurejea kwenye hali nzuri japo amekuwa akilalamika maumivu ya kichwa.

UKURASA. 23

# Kouame, Ngoma wasaini miaka miwili Simba

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Simba umetangaza kuwasainisha mikataba ya miaka miwili wachezaji wake wapya Aubin Kramo Kouame (27) kutoka Asec Mimosas ya Ivory Coast na Fabrice Ngoma kutoka klabu ya Al Hilal ya Sudan.

Kouame ambaye alitamba akiwa Asec kwenye michuano mbalimbali ya kimataifa kama Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, anamudu kucheza winga zote mbili pamoja na nafasi ya kiungo mshambuliaji, amekubali kusaini mkataba huo wa wekundu wa Msimbazi.

Hivi majuzi gazeti hili liliandika kuhusu Simba ilikuwa kwenye hatua za mwisho za kumsajili mchezaji huyo kwa gharama ya Sh. milioni 300 za Kitanzania ambazo zilikuwa za kuvunja mkataba na klabu yake ya Al hilal.

Jana kupitia mtandao wa Instagram, rasmi klabu hiyo ilimtambulisha mchezaji huyo na kuwa mmoja wa watakaovaa jezi nyekundu na nyeupe kwenye michuano yote ya ndani na nje ya nchi.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema umekuwa ni usajili wa kushtua akibainisha bado hawajamaliza kutangaza wachezaji wapya kwani wanataka kufanya maboresho makubwa kwenye kikosi cha msimu ujao.

Alisema Simba itanyakua kila mchezaji wanayemtaka kwenye mipango yao na wameanza na Ngoma na Kouame.

"Tuliwaahidi wanasimba kuwatangazia wachezaji wetu wapya, tumeanza sasa, Simba imefanya usajili wa akili nyingi, tutaendelea kuwachukua wachezaji wote ambao tunawataka na wapo kwenye mipango yetu," alisema Ahmed.

Historia ya Kouame inaonyesha alianza kucheza soka la ushindani kwenye klabu ya hiyo ya Asec Mimosas mwaka 2015, kabla ya kutimkia Africa Sports ya nchini humo mwaka 2017, hata hivyo miaka miwili baadaye aliondoka kwenye klabu hiyo akahamia FC San Pedro hapo hapo Ivory Coast alipocheza mpaka mwaka 2021 aliporejea tena Asec Mimosas kabla ya mwaka huu Simba kumsajili kwa ajili ya msimu ujao.

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >